Ministry of Foreign Affairs of Denmark
DANIDA | INTERNATIONAL DEVELOPMENT COOPERATION



# DENMARK – TANZANIA
# RASIMU YA SERA YA NCHI 2014-2018

# YALIYOMO


MUHTASARI WA UTENDAJI 3

1. DENMARK NA TANZANIA 5

2. CHANGAMOTO NA FURSA ZILIZOPO NA ZIJAZO KATIKA TANZANIA 7

3. MALENGO MKAKATI YA JUMLA NA MAENEO LENGWA YA DENMARK KATIKA USHIRIKIANO 16

4. KUONGEZEKA KWA USHIRIKIANO WA KUBADILISHANA UTAMADUNI 26

5. UTAFITI 26

6. MCHAKATO WA UFUATILIAJI 27

KIAMBATANISHO CHA 1
UKWELI KWA TANZANIA 28

KIAMBATANISHO CHA 2
SHUGHULI ZA MAENDELEO ZA DENMARK KATIKA TANZANIA 30

KIAMBATANISHO CHA 3
TATHMINI YA MAENDELEO MILLENIA KATIKA TANZANIA
BARA KUELEKEA MALENGO YA MAENDELEO YA 32

# MUHTASARI WA UTENDAJI

Tanzania imeonyesha mafanikio makubwa tangu ilipopata uhuru wake mwaka 1961. Ingawa Tanzania ni nchi yenye kipato cha chini, imeyapa kipaumbele maendeleo ya sekta za kijamii, kama vile upatikanaji wa maji safi, huduma za afya na hususan elimu ya msingi.

Sekta za uzalishaji kama vile kilimo na sekta binafsi hazikupewa kipaumbele katika ukuaji huo awali. Kwa hiyo, ukuaji katika sekta za uzalishaji umekuwa na matatizo ya kutokwenda sambamba na ongezeko kubwa la idadi ya watu katika Tanzania.

Matokeo ya Tanzania yanasisitiza kwamba uwekezaji katika watu na maendeleo ya watu yanahitaji ujuzi wa muda mrefu, angalau katika nchi kama Tanzania, iliyoanzia chini. Bado kuna sababu nyingi za kuendeleza ushirikiano wa karibu kati ya Denmark na Tanzania. Ushirikiano wa awali umeweka misingi imara ya ushirikiano , ambapo katika siku zijazo utajumuisha maeneo mapya kama uchumi wa kidiplomasia na ushirikiano wa kisiasa katika majukwaa ya kimataifa, juu ya masuala muhimu kama vile kupambana na uharamia, demokrasia na usalama.

Mambo mengi yamefanikishwa katika ushirikiano, na amani, ambayo imejengeka katika kipindi cha zaidi ya miaka 50 iliyopita, imeipa Denmark nafasi ya kipekee kutilia maanani na kudumisha jukumu kama mshirika muhimu ambaye kwa kushirikiana na Tanzania anaunga mkono katika kusaidia malengo ya maendeleo yaliyowekwa na Tanzania.




Map No. 3667 Rev. 6 UNITED NATIONS
January 2006

Department of Peacekeeping Operations
Cartographic Section

# 1. DENMARK NA TANZANIA

## 1.1 UTANGULIZI, MATOKEO NA DIRA IJAYO

Ushirikiano wa Denmark na Tanzania ni wa muda mrefu, imara na katika maendeleo endelevu. Tanzania ilikuwa nchi ya kwanza kwa Afrika ambayo Denmark ilianzisha ushirikiano wa msaada wa maendeleo mwaka 1963. Hii ilikuwa mwaka mmoja tu baada ya Bunge la Denmark (Folketinget) kupitisha sheria ya kwanza ya Denmark kuhusu ushirikiano wa kimataifa wa maendeleo na muda mfupi tu baada ya Tanzania Bara, iliyoitwa Tanganyika, kupata uhuru.

Zaidi ya miaka 50 iliyopita, Tanzania imepokea misaada zaidi ya maendeleo kutoka Denmark kuliko nchi nyingine yoyote, inayofikia kiasi cha zaidi ya Krona za Denmark (DKK) bilioni 14. Leo hii, Tanzania inaendelea kuwa mojawapo ya washirika wakuu wa misaada ya maendeleo ya Denmark na itabakia hivyo katika kipindi cha wastani. Katika kipindi chote cha miaka 50 ya ushirikiano, lengo kuu la ushirikiano wa maendeleo wa Denmark limekuwa ni kuchangia juhudi za Tanzania katika ujenzi wa taifa na katika mapambano yake dhidi ya umaskini uliokithiri.

Pamoja na misaada kutoka Denmark na kwa washirika wengine wa maendeleo kwa Tanzania, mafanikio mengi mazuri yameonekana. Hapa tunataja machache: Leo hii, Tanzania ni mojawapo ya nchi imara na yenye demokrasia ya amani zaidi katika Afrika, na mafanikio yake katika ujenzi wa taifa ni ya pili kipekee katika Afrika. Maboresho muhimu yameonekana katika sheria na mifumo ya taasisi kwa kukuza utawala bora, na vyama vya upinzani, vyombo vya habari, na asasi za kiraia zinazofanya kazi kwa uhuru zaidi leo kuliko wakati mwingine wowote katika historia ya Tanzania. Nchi hii, pia imepata uzoefu wa kuvutia na viwango imara vya ukuaji katika miongo iliyopita, kutokana na kiwango fulani cha usimamizi imara wa uchumi mkubwa na misaada kutoka kwa washirika wake wa maendeleo. Leo hii, Tanzania ni mojawapo ya nchi 20 duniani zenye uchumi unaokua kwa kasi.

Denmark imechangia katika jukumu la kuchochea maendeleo imara katika sekta ya fedha. Ukuaji imara wa uchumi wa Tanzania, ambao unatarajiwa kuongezeka kwa kasi kutokana na utajiri wa rasilimali zake za taifa, unaipa nchi misingi imara zaidi kuliko hapo awali inayohitajika kupunguza umaskini. Matokeo ya kuridhisha zaidi kutokana na ushirikiano wa muda mrefu, yanapatikana katika maeneo ambayo yamepata misaada zaidi ya maendeleo, na inaweza kuonekana katika uwezo wa upatikanaji wa huduma za jamii kwa wananchi. Msaada mkubwa kutoka Denmark na kutoka kwa washirika wengine umesaidia upanuzi wa haraka na wa kina wa idadi kubwa ya watu kupatiwa huduma za kijamii kama vile afya, elimu na upatikanaji wa maji safi. Maendeleo haya yamesababisha matokeo imara katika mapambano dhidi ya umaskini kwa mtazamo mpana. Umaskini si wa kiuchumi tu pia unahusisha ukosefu wa upatikanaji wa huduma za jamii kama vile afya na elimu. Kwa ujumla, uzoefu wa miaka 50 ya ushirikiano ni mzuri, na kuna msingi thabiti kwa ajili ya ushirikiano wa baadaye.

Uhitaji wa kuendelea kushirikiana zaidi na msaada wa kimaendeleo ni dhahiri. Tanzania, inaendelea kuwa mojawapo ya mataifa mengine maskini zaidi duniani. Karibu theluthi moja ya watu wake wanaishi katika umaskini uliokithiri, na kukosekana kwa usawa unaopimwa kwa kipato na katika upatikanaji wa huduma bora za jamii, unaokua kwa kasi. Kufanikisha dira ya Serikali ya Tanzania ya kufikia kiwango cha hadhi ya kipato cha kati ifikapo mwaka 2025, itahitaji juhudi imara na zenye ubunifu. Tanzania iko njia panda, na katika miaka kumi ijayo itakuwa na hali mbaya sana katika mstakabali wa baadaye wa nchi. Maamuzi yaliyofanywa yataamua mgawanyo wa mapato na rasilimali kwa vizazi vijavyo, na kama maamuzi sahihi hayatafanywa, yataisababishia nchi changamoto katika uwepo wa utamaduni wa amani wa muda mrefu, kati ya makundi mbali mbali ya kikabila na ya kidini.

## 1.2 DIRA YA KUENDELEZA USHIRIKIANO

Katika miaka 50 ya matokeo mazuri na uihitaji mkubwa wa kuendelea kusaidiwa, Denmark itaendelea kuwa mshirika muhimu wa Tanzania. Rasimu hii ya mkakati wa nchi, inawasilisha maoni ya serikali ya Denmark kuhusu changamoto zilizopo na zinazojitokeza na fursa zilizopo kwa Tanzania, pamoja na malengo mkakati ya kuendeleza ushirikiano na maeneo lengwa yaliyochaguliwa kwa ajili ya ushirikiano.

Kwa ujumla, dira ya baadaye ya ushirikiano na Tanzania ni kuwawezesha watanzania wote kushiriki kikamilifu, katika maendeleo ya nchi na kuhakikisha inasimamia uendelezaji wa historia yake ya muda mrefu ya uwepo wa amani, demokrasia na maendeleo. Pamoja na lengo hili la ujumla, malengo mkakati matatu makuu ya ushirikiano ya Denmark kwa Tanzania ni kuisaidia na kukuza juhudi za serikali ya Tanzania za:

1. Kupunguza umaskini na ukosekanaji wa fursa sawa na kuhakikisha upatikanaji wa huduma bora za kijamii,

2. Kukuza uchumi wa kijani na ajira,

3. Kuimarisha demokrasia,utawala bora, utawala wa sheria na kuheshimu haki za binadamu kwa wote.

Ili kufikia malengo mkakati haya, kipaumbele kitatolewa ili kufikia matokeo halisi katika maeneo lengwa yafuatayo:

a. Sekta ya afya,

b. Sekta ya kilimo,

c. Mahitaji ya kuhakikisha utawala bora na haki za binadamu kwa wote

d. Ukanda wa amani na uthabiti.

Ushirikiano katika maendeleo utaendelea kuwa suala muhimu la ushirikiano, lakini msaada wa Denmark kwa maendeleo lazima utekeleze jukumu la kuchochea katika kukuza mabadiliko muhimu ya maendeleo katika maeneo muhimu na kushawishi mifumo mingine ya umma na misaada ya kibinafsi katika ushirikiano. Kwa nyongeza, ushirikiano kati ya Denmark na Tanzania utaimarishwa katika maeneo mengine, hasa kwenye mahusiano ya kibiashara na ushirikiano wa kisiasa, kikanda na kimataifa.

# 2. CHANGAMOTO NA FURSA ZILIZOPO NA ZIJAZO KATIKA TANZANIA

Katika miaka ya hivi karibuni, Tanzania imepata maendeleo makubwa ya kisiasa, kiuchumi na maboresho katika ustawi wa jamii. Hata hivyo, nchi inaendelea kukabiliana na changamoto muhimu za maendeleo, si tu katika maeneo muhimu kama; mgawanyo wa kiuchumi, ongezeko la idadi ya watu, rushwa, na mgawanyiko mkubwa kati ya vyama na dola. Wakati huo huo, fursa mpya zinajitokeza ambazo zina uwezo wa kutoa maamuzi kwa ajili ya mabadiliko muhimu na mageuzi.

## 2.1 UMASKINI NA UKOSEFU WA FURSA SAWA: UKUAJI MKUBWA WA UCHUMI, USIOKUWA WA WOTE

Tanzania imekuwa na historia ya mafanikio makubwa ya uchumi takribani kwa miongo miwili. Kiwango cha ukuaji wa uchumi kimeongezeka kutoka asilimia tatu nukta tano (3.5%) katika miaka ya 1990 hadi asilimia saba (7%) katika miaka ya 2000. Licha ya kuyumba kwa uchumi duniani, viwango vya ukuaji vimeendelea kuwa imara katika muongo uliopita, na unatarajiwa kuendelea au kuongezeka katika matazamio ya siku zijazo. Wakati huo huo, nchi imekabiliwa na ongezeko kubwa la idadi ya watu kutoka watu milioni 11 mwaka 1963 na kufikia takribani watu milioni 45 mwaka 2012. Ongezeko la idadi ya watu limebaki kuwa juu, karibu ya asilimia tatu (3%) kwa mwaka. Kama ongezeko hili kubwa litaendelea, kutakuwa na watanzania milioni 53 mwaka 2018 na milioni 100 mwaka 2042.

Ukuaji wa uchumi na miongo ya muda mrefu ya misaada ya kimataifa imesababisha matokeo mazuri, lakini ni muhimu kukumbuka kuwa ukuaji wa uchumi huanzia katika hali ya chini sana na umaskini huo kwa Tanzania umeonyesha changamoto kubwa kupita kiasi. Na Pato la Taifa kwa kila mtu (per capita) kwa mwaka la dola 532 (2011), na kielelezo cha uwiano maendeleo ya binadamu kinaiweka Tanzania katika nafasi ya asilimia 20 (20%) ya kiwango cha chini kwakuwa  Tanzania ni mojawapo kati ya nchi 15 maskini zaidi duniani. Zaidi ya theluthi mbili ya idadi ya watu wanaishi chini ya kiwango cha chini cha umaskini kinachotambulika kimataifa cha dola za Kimarekani 1.25 kwa siku, na karibu asilimia tisini (90%) wanaishi chini ya dola mbili kwa siku. Takribani theluthi moja wanaishi chini ya “mstari wa mahitaji ya msingi ya umaskini” unaolingana na karibu dola za Kimarekani 0.96 kwa siku.[1] Kwa kutumia Kipimo hiki tu, viwango rasmi vya umaskini vilipungua kidogo kutoka asilimia thelathini na tisa (39%) ya idadi ya watu mwaka 1992 hadi asilimia thelathini na nne (34%) mwaka 2007, mpaka asilimia ishirini na nane (28%) mwaka 2012. Kutokana na ukuaji wa idadi ya watu, hata hivyo, uwiano huu wa kupungua bado unamaanisha idadi halisi ya watu wanaoishi chini ya mstari wa umaskini imebakia katika kiwango kile kile cha watanzania milioni 11-12. Tafiti rasmi zinaonyesha kiwango kisichobadilika cha ukosekanaji wa fursa sawa kuanzia mwaka 2001 hadi 2007 (Gini 0.35). Mahesabu mengine yalionyesha ongezeko la asilimia ishirini (20%) la uwiano usio sawa katika kipindi hicho hicho.[2] Kiwango cha ukosekanaji wa fursa sawa kinaweza kuonyeshwa kwa ukweli kwamba asilimia ishirini (20%) ya watu matajiri katika Tanzania wanahesabika kutumia asilimia arobaini na mbili, wakati asilimia ishirini (20%) ya watu maskini wanatumia asilimia saba (7%) tu.

Njia ya wastani ya kupunguza umaskini inaonyesha kwamba ukuaji wa uchumi haujakua vizuri kwa kiwango kikubwa. Ukuaji umejikita katika mawasiliano ya simu, huduma za fedha, biashara ndogo ndogo, madini, utalii, ujenzi na viwanda. Wakati hapo mwanzo ukuaji wa uchumi ulisukumwa zaidi na matumizi ya umma na misaada ya kimataifa, jambo ambalo kwa sasa halipo tena. Ukuaji wa uchumi sasa unatokana hasa na sekta binafsi, lakini sekta zenye viwango vya juu vya ukuaji zimewekeza kwa makini na kujikita katika maeneo ya miji mikubwa. Ukuaji wa umeshindwa kwa kiasi kikubwa

1. Katika ripoti ya bajeti ya kaya, serikali ya Tanzania inatumia kipimo tofauti cha umaskini kuliko kiwango cha kimataifa cha PPP cha dola1.25 kwa siku. Kipimo cha serikali kinaegemezwa kwenye matumizi na kinatafuta kuonyesha uwiano wa idadi ya watu ambao hupata mahitaji yao ya kila siku. Kinalingana na PPP dola 0.96 kwa siku.
2. Kiwango cha “Theil”kinaonyesha ongezeko la asilimia kumi na tisa (19%) katika ukosefu wa usawa, na wino wa “palma” unaonyesha ongezeko la asilimia ishirini na moja nukta nane(21.8%). ukokotoaji wote unaegemezwa kwenye takwimu ya ripoti ya bajeti ya kaya kama ulivyo ukokotoaji wa “Gini Coeffient.”

kukabiliana na changamoto kubwa, kuongeza nafasi zaidi za ajira na kazi zaidi katika maeneo yote ya jamii na kuboresha kipato kwa idadi kubwa ya watu.

Moja ya sababu kubwa ya kushindwa kupunguza umaskini, licha ya ukuaji wa uchumi ni kwamba Tanzania haijafanikiwa kuinua kiwango cha uzalishaji katika kilimo kwa miongo iliyopita. Tanzania bado inaendelea kutegemea kilimo, ikiwa robo tatu ya wakazi wake wanaishi katika maeneo ya vijijini. Asilimia themanini ya watanzania maskini wanaishi katika kaya za vijijini. Ukuaji katika sekta ya kilimo umebaki kuwa chini kwa takribani kiasi cha asilimia nne (4%) kwa mwaka, na katika maeneo ya vijijini ukuaji wa uzalishaji ni mdogo sana kulingana na oongezeko la watu. Viwango vya uzazi katika maeneo ya vijijini vikubwa (vizazi 6.1 kwa mwanamke ikilinganishwa na 3.7 katika maeneo ya mijini).

Wakati wafadhili na serikali wametumia rasilimali muhimu katika kuboresha sekta za jamii, msaada wa aina hiyo haujatolewa kwa sekta ya kilimo na sekta nyingine za uzalishaji. Ukosekanaji wa hati za kumiliki ardhi, ili kuhakikisha kwamba watumiaji wa kijadi katika maeneo ya vijijini hawapotezi ardhi yao ambayo ni mojawapo ya masuala muhimu, yanayokwamisha uwekezaji unaoweza kuongeza tija katika uzalishaji. Usindikaji wa chakula na mazao mengine ya kilimo, na pia aina nyingine za uzalishaji ni mdogo sana katika maeneo ya vijijini, kwa hiyo yana mchango mdogo sana katika kuongeza fursa za ajira.

Kwa sababu hiyo, Tanzania inakabiliwa na wimbo la vijana kuhama kutoka kwenye maeneo yenye uzalishaji mdogo wa kilimo kwenda mijini kwenye sekta zisizo rasmi, ambapo pia uzalishaji ni mdogo. Ukosefu wa ajira ni mkubwa, na unaongezeka kwa kasi miongoni mwa vijana, hususan katika maeneo ya mijini. Kiwango rasmi cha ukosefu wa ajira ni asilimia kumi na mbili (12%) na ni kikubwa katika miji mikubwa, na ilifikia asilimia thelathini na mbili (32%) kwa Dar es Salaam (2006). Aidha, theluthi moja ya walioajiriwa wanajulikana kama “vibarua”: wanaajiriwa kijanja, na kipato chao kiko chini ya mstari wa mahitaji ya msingi ambayo ni dola za Kimarekani 0.96 kwa siku. Mara nyingi hufanya kazi za mashambani au katika sekta zisizo rasmi zenye uzalishaji mdogo mijini na ajira za muda mfupi. Inakadiriwa kuwa vijana wapya 700,000 wanaotafuta kazi huingia katika soko la ajira kila mwaka, lakini ni sehemu ndogo tu ya wenye uwezekano wa kupata ajira ya uhakika ambayo inawapa uwezekano wa kuhudumia familia. Ongezeko la wanaohama kutoka vijijini kwenda mijini litaendelea kwa miaka ijayo, na tayari Dar es Salaam umekwishakuwa mojawapo ya miji inayokua kwa kasi Barani Afrika.

Katika tofauti kubwa ya kukithiri kwa umaskini Tanzania imeshuhudia utokeaji wa kundi dogo, lakini linalopanuka na kuwa tabaka la kati mijini. Ni kundi dogo sana, la karibu asilimia kumi (10%) tu ya idadi ya watu, lakini lina nguvu ya manunuzi inayokua, ushawishi mkubwa wa kisiasa, na limeweka mahitaji ya kisiasa na kiuchumi- upatikanaji wa umeme wa bei nafuu, bidhaa za kutoka nje, kutoa huduma bora za kijamii mijini, na miundombinu katika maeneo ya mijini. Serikali inafanya juhudi kukidhi matakwa haya, kwa mfano, kupitia ruzuku kubwa kwa ajili ya umeme wa bei nafuu, misamaha mikubwa ya kodi kwa makampuni ya kigeni na ya ndani, pamoja na watumishi wa serikali, na kwa sehemu kubwa malipo ya posho za kukijikimu zisizo kuwa na kodi kwa watumishi wa umma. Jitihada hizi za serikali zinajaribu kuridhisha tabaka la kati badala ya kupunguza, fursa isiyosawa katika jamii. Hii inaweza kutishia kuendelea kwa amani na uthabiti pamoja na mshikamano wa kijamii kwa Tanzania.

Uvumbuzi wa hivi karibuni wa akiba ya gesi asilia umekuwa nyongeza katika rasilimali kubwa ya madini iliyopo. Matarajio ya muda mrefu ya uchumi wa Tanzania yanaonekana kutoa matumani na tayari rasilimali hizi zimewavutia wawekezaji wa kigeni. Hata hivyo, faida zinazoweza kupatikana kutokana na utumiaji wa maliasili kwa kiasi kikubwa hautafanikiwa kwa miaka mingine10 au zaidi, na ni muhimu sana kuhakikisha kuna usimamizi wa uchumi mkubwa. Kwa miaka ya karibuni, serikali imeongeza matumizi yake ya riba pamoja na mikopo yenye masharti nafuu. Kutokana na

ongezeko la ukopaji, deni la taifa la Tanzania limeongezeka kutoka asilimia ishirini na nane (28%) hadi asilimia arobaini (40%) ya Pato la Taifa katika miaka minne tu. Deni linaendelea kukua kwa kasi, ikilinganishwa na ongezeko la ulipaji wa madeni na marejesho. Uwezo wa nchi kifedha wa nchi haujatikiswa, lakini usimamizi wa madeni umezidi kuwa muhimu zaidi, na kuna haja kubwa ya uimarishaji wa kudhibiti uwekezaji wa umma. Kuna uhitaji maalumu wa uwazi zaidi katika mikataba ya umma na manunuzi.

## 2.2 MAENDELEO YA JAMII

Umaskini hauwezi kupimwa kirahisi tu kwa kuangalia mgawanyo wa mapato na ugawaji wa rasilimali peke yake. Takwimu rasmi zinalenga tu katika matumizi binafsi na kwa hiyo zinakadiria chini ya kiwango umuhimu wa utumiaji wa bidhaa zinazotumiwa na umma. Takwimu kwa hiyo, zinakadiria chini ya kiwango mafanikio yaliyopatikana katika miaka ya hivi karibuni. Serikali ya Tanzania imechagua kutumia rasilimali muhimu katika kutoa mahitaji ya bidhaa kwa watu wake. Matokeo yake upatikanaji wa maji safi, elimu na huduma za afya zimeboresha kwa miongo iliyopita. Kwa matokeo hayo, Tanzania imepanda hadi kufikia nafasi ya saba katika kielelezo cha Maendeleo ya Binadamu (HDI) kutoka mwaka 2006 hadi 2013, kielelezo kilichochapishwa na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP). Tanzania pia imepiga hatua katika juhudi zake za kufikia Malengo ya Maendeleo ya Milenia ya Umoja wa Mataifa (MMMUM).

Tanzania imeweka msisitizo maalumu kwenye elimu, na maboresho makubwa yamefanyika kuwawezesha wananchi wengi kupata elimu ya msingi. Leo hii, Tanzania ni moja ya nchi chache yenye kipato cha chini ambayo inakaribia kufanikisha elimu ya msingi kwa wote. Pia mafanikio yamepatikana katika juhudi za kupunguza tofauti kati ya wasichana na wavulana katika upatikanaji wa elimu na katika mapambano dhidi ya VVU / UKIMWI, malaria na magonjwa mengine kadhaa. Katika sekta ya afya, mafanikio ya jumla yamepatikana katika kuendeleza upatikanaji wa huduma za msingi za afya, na matokeo yake yameonekana katika ongezeko la idadi ya watoto wanaoishi. Kumekuwa na kushuka kwa idadi ya vifo vya watoto wachanga (kiwango rasmi cha vifo vya watoto), pamoja na vifo vya watoto walio chini ya umri wa miaka mitano. Hata hivyo, kumeendelea kuwa na changamoto kubwa za kupunguza vifo vya uzazi. Matumizi ya serikali kwa upande wa elimu yameongezeka kwa kiasi kikubwa katika miaka ya hivi karibuni, ambapo matumizi ya afya yamepungua, katika thamani halisi na kama mgawanyo katika bajeti ya taifa.

Katika sekta zote za kijamii, kuna mahitaji makubwa endelevu katika kuongeza ubora wa huduma zinazotolewa. Upanuzi mkubwa wa kujaribu kumfikia kila mmoja kwa huduma za elimu na afya, umepunguza ubora wa huduma katika nyanja zote. Tafiti za hivi karibuni zinaonyesha kwa kina na kuendelea kuwepo kwa matatizo ya ubora wa elimu ya msingi na sekondari kwa pamoja, matokeo yake ni kuwa wanafunzi wanamaliza shule bila ujuzi wa kutosha. Katika mwaka 2012, asilimia sitini (60%) ya wanafunzi hawakufaulu mtihani wa Taifa wa kidato cha nne.

Ubora wa huduma ya afya ya msingi umeathiriwa na sababu mbalimbali, ikiwa ni pamoja na uhaba na usambazaji mbaya wa wafanyakazi wa afya, upatikanaji mbovu wa dawa muhimu na miundombinu mibovu. Hali hii, ina athiriwa zaidi na ongezeko la kasi la idadi ya watu. Moja ya viashiria vinavyoonesha kuwa ubora wa huduma za afya ni duni unaonekana katika ongezeko dogo la idadi ya wajawazito ambao hujifungua katika vituo vya afya. Mwaka 2004, asilimia arobaini na saba (47%) ya wanawake wajawazito walijifungua katika vituo vya afya vya umma. Miaka sita baadaye, mwaka 2010 uwiano ulikuwa umeongezeka hadi kufikia asilimia hamsini (50%) tu.

Katika miaka iliyopita, Serikali ya Tanzania imefanikiwa kupunguza nafasi zilizokuwa wazi za wafanyakazi wa afya kutoka asilimia sitini na tano (65%) mwaka 2007 hadi asilimia arobaini na moja (41%) mwaka 2011. Haya ni maboresho muhimu yakuonekana, lakini bado ni kama nusu tu ya nafasi zilizojazwa. Upatikanaji

wa huduma za kijamii umeendelea kutogawanywa kwa uwiano sawa. Kwa vyote, yaani afya na elimu, kuna tofauti za wazi katika njia za kupata huduma na katika ugawanywaji wa matumizi ya umma kwa vikundi tofauti katika jamii. Hii inahusu tofauti kati ya maskini na tajiri, ambapo mmoja anaishi katika nchi yenye tofauti kati ya maeneo ya vijijini na mijini. Kwa mfano, idadi ya wauguzi katika huduma za afya kwa kila mtu ni mara 30 zaidi katika wilaya zenye nafasi bora zaidi ya zile zisizokuwa nazo. Zaidi ya nusu ya madaktari bingwa hufanya kazi Dar es Salaam. Kwa hiyo, haishangazi kuona kwamba uwiano wa idadi ya wanawake wajawazito ambao huchagua kwenda kujifungulia katika vituo vya afya ni kubwa mara 3 zaidi kuliko maeneo mengine ya nchi. Hii inaonyesha ni jinsi gani ilivyo muhimu kuwa na mtazamo thabiti katika kuboresha ubora na fursa sawa katika huduma za jamii. Vigezo hivi vinaonyesha kwa namna moja au nyingine havikutiliwa maanani ili kufikia Malengo ya Maendeleo ya Milenia (MMMUM) kwa viwango vingi vinavyowezekana kufikiwa.

## 2.3 AMANI, UTHABITI NA DEMOKRASIA

Tanzania - pamoja na demokrasia yake vya vyama vingi na kutotawaliwa kidini imeendelea kuwa nchi imara katika ukanda wenye mabadiliko. Miaka hamsini ya amani na mshikamano bila vita vya wenyewe kwa wenyewe, migogoro ya kijeshi au mapinduzi ya kijeshi, imekuwa kivutio. Rekodi hii, pamoja na mchango wa kihistoria wa Tanzania kwa Paafrika (Pan Africanism) na kusaidia vikundi mbalimbali vya ukombozi katika bara la Afrika, ni kigezo muhimu katika kuelezea kwa nini nchi imekuwa mchangiaji mkubwa katika ulingo wa siasa katika Afrika. Kwa kiwango kikubwa Baba wa Taifa Nyerere na chama tawala Chama cha Mapinduzi (CCM) wanahusika na wanaweza kusifiwa katika kuweka misingi ya kipekee na ya amani katika kujenga taifa la kiafrika. Kihistoria, Tanzania inatambulika kwa kuwa na uhuru wa kuabudu, na utamaduni imara na wa muda mrefu wa uvumilivu na amani na mshikamano kati ya imani tofauti na vikundi vya jadi. Kwa hiyo, historia yake kama taifa la chama kimoja na mpaka leo, zaidi ya miaka 20 baada ya kuanzishwa demokrasia ya vyama vingi, mchakato wa kutenganisha serikali na chama bado haujakamilika, na hii ni changamoto mojawapo kubwa kwa taifa laTanzania.

Chama tawala, CCM, kimetawala nchi tangu uhuru na kinaendelea kufurahia kwa kuwa na viti vingi bungeni. Hata hivyo, uungwaji mkono wa vyama vya upinzani umeendelea kuimarika katika miaka ya hivi karibuni, kutokana na migogoro ya ndani CCM na kutoridhika kwa umma kutokana na maendeleo hafifu katika kushughulikia changamoto za kijamii na za kiuchumi. Ingawaje Tanzania imeendelea kupanua mfumo wa vyama vingi, ni vigumu kufikiria kwamba chama cha CCM ambacho kimekuwa kikishikilia madaraka kinaelekea kutikiswa vibaya katika muongo huu. Licha ya utendaji wa kiuchumi wa Tanzania, CCM imekuwa daima na msingi imara zaidi katika maeneo mengi ya vijijini, na ni vigumu kwa vyama vingine vya kisiasa kuwa na athari kwa maeneo hayo. Mengi yatategemea ni kwa namna gani chama kitaweza kukabiliana na hali ya kukatisha tamaa, inayoongezeka hususan, miongoni mwa vijana.  Hali hii ya kukatisha tamaa, imetengeneza mazingira mazuri kwa siasa za ushindani zaidi, kupungua kwa uthabiti, na kupungua kwa viongozi wanaotaka maelewano ambao Tanzania imekuwa ikiwaandaa. Kwa sasa kumekuwa na matukio mengi ya uadui ulio wazi na migongano mikali kati ya vyama vya siasa, vikundi vya dini na wenye mamlaka kuliko ilivyokuwa hapo awali. Pia kumekuwa na migomo ya watumishi wa umma, na migogoro ambayo haikuwahi kuwepo Tanzania katika muongo mmoja uliopita imeendelea kutokea mara kwa mara.

Kwa ujumla, Tanzania ina uhusiano mzuri na karibu nchi zote zilizo jirani nayo, na hakuna tishio kubwa kwa nchi. Shughuli za uharamia nje ya mwambao wa pwani ya Afrika Mashariki zimepungua kwa kiwango kikubwa ikilinganishwa na kiwango cha mwaka 2010, kutokana na kuongezeka kwa uwepo wa jeshi la wanamaji la kimataifa na ongezeko la matumizi ya mfumo wa ulinzi binafsi. Hata hivyo, uharamia umeendelea kutoa tishio kubwa kwa usafiri wa baharini kutoka na kuingia Tanzania, hivyo kuathiri nchi jirani zisizo na bandari ambazo pia zinahudumiwa na bandari ya Dar es Salaam.

## 2.4 ZANZIBAR: MTAZAMO PEKEE KUHUSU ZANZIBAR

Uhusiano tata kati ya eneo lenye uhuru nusu la Zanzibar, na muungano ambao unajumuisha Tanzania ni mada muhimu katika siasa za ndani za Tanzania, si jambo dogo katika mazingira ya mabadiliko ya Katiba. Wazanzibari wengi wanashauku kubwa ya kuongezeka kwa uhuru wa Zanzibar. Muundo uliopo ambapo muungano una jukumu katika maeneo muhimu kama vile ya mambo ya nje, na sera ya usalama, inaendelea kukabiliana na ongezeko la umaarufu wa upinzani. Kutokana na umuhimu wa uhifadhi wa gesi katika ukanda wa bahari ya Zanzibar, kuna hali maalumu ya kutokuridhika kwamba muungano pia una jukumu la jumla katika maliasili hiyo.

Chama cha Wananchi (CUF) kimekuwa chama kikuu cha upinzani Zanzibar, lakini katika mwaka 2010 kiliingia katika serikali ya umoja wa kitaifa na CCM. Wakati serikali mwanzoni iliridhishwa na uungwaji mkono imara, ushirikiano kwa sasa unaonekana kama usio na ufanisi. Wakati huohuo ushiriki wa CUF katika serikali umedhoofisha uungwaji mkono ndani ya chama. CUF inakabiliwa na migogoro ya ndani na ombwe la kisiasa katika siasa za upinzani limejitokeza. Wanaharakati wanatafuta kuziba ombwe hili, na kuna hatari kuwa medani za kisiasa Zanzibar zitachukuliwa na asasi zenye utetezi mkali, kama vile kuongezeka kwa harakati za umaarufu wa kundi la Uamsho, ambalo hukuza kanuni za kiislamu na uhuru kamili kwa Zanzibar. Kwa hiyo, Zanzibar imeshuhudia kuongezeka kwa wasiwasi wa kidini, na matukio kadhaa ya machafuko, kati ya vikundi vyenye msimamo mkali wa kiislamu na mamlaka husika. Maboresho ya katiba yanatarajiwa wakati tume ya serikali itakapowasilisha ripoti yake mwishoni mwa 2013, yanaweza kuipa uhuru zaidi Zanzibar, na mabadiliko zaidi ya kisiasa yanajenga mabadiliko muhimu hali ya uchumi wa Zanzibar, hasa kama mabadiliko yataleta ukomo wa mazoea ya kupewa ruzuku kutoka bajeti ya muungano.

## 2.5 HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA WA KISHERIA

Kutokana na mtazamo kikanda, Tanzania imeendelea kuwa na rekodi chanya ya haki za binadamu. Tanzania imeridhia vyombo vyingi vya kimataifa kuhusu haki za binadamu, na kuanzisha mifumo ya taasisi za kusaidia utawala wa kidemokrasia, na utekelezaji wa haki za binadamu. Baada ya mapitio ya mara kwa mara ya haki za binadamu ya Umoja wa Mataifa yaliyofanyika 2011, serikali ya Tanzania iliafiki mapendekezo kadhaa yaliyotolewa.

Hii inaonyesha ishara ya serikali ya Tanzania kuendelea kutekeleza uboreshaji wa hali ya haki za binadamu. Hata hivyo, licha ya mfumo chanya kuna masuala muhimu katika wigo wa uboreshaji wa hali halisi za haki za binadamu kwa ujumla.

Katiba inatoa haki za msingi kwa raia na za kisiasa ikiwemo uhuru wa kukusanyika na kuongea. Asasi za kijamii na vyombo vya habari vimetoa mchango mkubwa katika siasa za ndani kwa miaka ya hivi karibuni, na hili limesababisha kuongezeka kwa ufuatiliwaji wa vyombo vya habari na serikali. Hata hivyo, uhuru wa kujieleza, upatikanaji wa habari na uhuru wa vyombo vya habari unaongozwa na sheria zilizopitwa na wakati, ambazo huiwezesha serikali kuyafungia kwa vipindi mbalimbali magazeti yanayoikosoa. Udhibiti binafsi pia unakuwepo. Mahakama imebaki kuwa huru kwa kiasi kikubwa, lakini pamekuwepo na maoni kuhusu matukio ya Tanzania kutofikia viwango vya kimataifa katika utoaji wa hukumu za haki, ambapo rushwa inaendelea kuwa changamoto kubwa. Ukosefu wa uwezo na vikwazo vya rasilimali, pamoja na sheria ni vikwazo vingine kwa wananchi wengi kupata huduma bora ya utawala wa kisheria, kwa kuzingatia muda muafaka na uamuzi wa haki wa kesi zao. Aidha, kuna matukio ya mara kwa mara ya watu kujichukulia sheria mkononi yanayosababisha mauaji.

Wakati ambapo juhudi zimefanywa kukuza utekelezaji kwa vitendo vya kiuchumi, haki za kijamii na utamaduni, utambuzi wa haki hizi unaendelea kuwa changamoto kubwa. Ukosefu wa ajira uko juu, na viwango vya kimataifa vya kazi havitekelezwi kwa ufanisi. Tafauti za uwiano wa kijinsia zimekitwa ndani ya mfumo wa tamaduni za kijamii, na ukatili dhidi ya wanawake na watoto pamoja na unyanyasaji wa

majumbani, ukeketaji wa wanawake na utumikishwaji wa watoto unaendelea kuongezeka kwa kiwango kikubwa. Kuna ongezeko kubwa pia linaloendelea la ukosefu wa usalama wa kujamiiana na haki ya uzazi, na matokeo yake ni kuendelea kuongezeka kwa kiwango kikubwa cha mimba zisizotarajiwa, vifo vya watoto chini ya miaka 5 na vya uzazi. Pia kuna viwango vikubwa vya mimba za utotoni, na wanawake wanakosa taarifa na msaada wa uzazi wa mpango, pamoja na huduma nyingine za afya ya uzazi.

Zaidi ya hayo, vikundi vya watu wachache kama (wasagaji na mashoga), na watu wenye ulemavu wa ngozi (albino) wanaendelea kubaguliwa katika jamii ya Tanzania.

## 2.6 UTAWALA BORA, UWEZO WA SEKTA ZA UMMA NA MATATIZO YA RUSHWA

Katika suala la utawala bora, Tanzania imepata kiwango cha wastani katika ulinganisho wa kimataifa. Dalili mojawapo ya maendeleo ni kwamba wananchi wameanza kupata utambuzi na ushawishi kuliko ilivyokuwa hapo awali. Wananchi, bunge, vyombo vya habari na asasi za kijamii zinaendelea kuitaka serikali iwajibike kikamilifu, na iwajibike kwa wananchi. Tanzania pia hivi karibuni imeona maendeleo ya uwazi katika bajeti na watu kuweza kupata habari, lakini mazingira ya kisiasa yanaendelea kutawaliwa na mfumo wa juu-chini.

Serikali imekuwa ikipewa changamoto za mara kwa mara katika masuala ya ufanisi, utawala wa sheria, na mapambano dhidi ya rushwa yanaendelea kuwa moja ya changamoto kubwa ya Tanzania. Miongo ya mageuzi katika sekta za umma yameiwezesha Tanzania kupata mafanikio bora kuliko nchi nyingine za Afrika katika usimamizi wa fedha za umma (PFM). Sheria mbalimbali, vyombo vya udhibiti na mifumo imewekwa na kutekelezwa katika kipindi cha zaidi ya miaka 15 iliyopita. Kanuni za ununuzi ni za kiwango cha kimataifa, lakini zinaendelea kuwa na changamoto za kuhakikisha zinaendana na viwango hivyo. Bajeti za umma zimekuwa wazi zaidi, lakini ushiriki wa wananchi katika masuala haya umeendelea kuwa wa kawaida. Uwezo wa usimamizi wa ofisi ya ukaguzi wa mahesabu ya ndani unaendelea kuboreshwa na ripoti zake zinajadiliwa miongoni mwa wananchi na katika bunge, lakini ufuatiliaji wa mapendekezo ya ukaguzi wa mahesabu unaendelea kuwa changamoto.

Zaidi ya muongo mmoja uliopita, serikali imefanikiwa katika kuongeza ushuru wa mapato, kupitia ufanisi wa usimamizi wa kodi. Makusanyo yanawiana na asilimia kumi na nane (18%) ya pato la taifa, ambayo ni ya juu kwa viwango vya Kiafrika. Changamoto ya baadaye ni kuboresha sera za kodi ili mzigo wa kodi ugawanywe kwa upana zaidi katika jamii. Changamoto ya kipekee ni ya kiwango kikubwa cha misamaha ya kodi, inayokadiriwa kusababisha upotevu wa kiasi cha asilimia nne (4%) ya pato la taifa kwa mwaka. Aidha, utata na kutokuwa na mfumo usio wazi wa misamaha ya kodi unachangia kuwepo kwa rushwa. Urekebishaji wa mfumo na kupunguza idadi ya misamaha ya kodi unahitaji ufundi wa kina, juhudi na uwezo wa kitaalamu, lakini utashi wa kisiasa na utatuzi vina umuhimu sawa.

Rushwa imeendelea kubaki kuwa changamoto kubwa kwa Tanzania katika nyanja zote za utawala bora, na katika maendeleo yote ya kijamii. Kiwango kidogo na kikubwa cha rushwa kilichobainishwa na tafiti za kimataifa, na tafiti za ndani, vimeendelea kuhusika kwa kiwango kikubwa na kuathiri sekta zote za kiuchumi, kwa huduma zote za umma zinazotolewa katika uendelezaji wa rasilimali, uzalishaji wa viwandani na biashara. Mfumo halali wa uzuiaji wa rushwa na Taasisi ya kuzuia rushwa katika Tanzania vinaweza kulinganishwa na zile za kutoka nchi nyingine za Kiafrika. Hata hivyo, kwa utaratibu, inapaswa uwepo uwezekano mzuri wa kuhimiza mapambano yenye tija dhidi ya rushwa, lakini hili linahitaji ushirikiano thabiti wa kisiasa na kuongeza ushirikiano zaidi na vyombo vya habari, asasi za kiraia na bunge. Kumekuwapo na mafanikio chanya katika miaka ya hivi karibuni, bali changamoto kubwa zimebaki katika utekelezwaji na usimamizi wa sheria. Pamoja na hayo, tatizo kubwa ni kwamba ni kesi chache tu za rushwa zimehukumiwa katika mahakama.

Fursa kuu mpya na mipango mipya inaanzishwa. Hatua zimechukuliwa katika kutekeleza sheria, na kufikia kiwango kilichowekwa na mashirika kama vile, mpango wa uzinduzi wa uwazi kwa viwanda (EITI) ulioanzishwa). Hili linawezesha kuimarisha mapato ya ndani na usimamizi wa fedha, na maendeleo chanya ndani ya mabadiliko ya PFM. Hata hivyo, ni muhimu sana, kuendelea kuimarisha mfumo na utaratibu wa uwazi, uwajibikaji na uwazi katika mfumo wa kiraia.

## 2.7 USIMAMIZI WA MALIASILI

Tanzania ni nchi yenye utajiri wa maliasili na ni nchi mojawapo yenye maeneo makubwa ya misitu katika nchi za Afrika Mashariki, na Kusini mwa Afrika. Utajiri wa mbuga za wanyama pamoja na kukua kwa kasi kwa sekta ya utalii, unachangia kiasi cha asilimia kumi na nane (18%) ya Pato la Taifa. Uchimbaji wa madini umedhukuliwa kwa kiwango cha juu sana, lakini kiwango cha ukuaji kinachobadilika badilika katika muongo mmoja uliopita kwa kiwango cha ukuaji wa asilimia kumi na tano (15%) kwa mwaka. Hata hivyo, izingatiwe kwamba idara za ukuaji kutoka kiwango cha chini na uchimbaji wa madini unachangia chini ya asilimia tano (5%) ya pato la Taifa. Serikali inatarajia kwamba sekta ya madini itaongezeka kwa kiasi cha asilimia kumi (10%) cha pato la Taifa ifikapo mwaka 2025. Maliasili tayari zinahesabika kuwa na uwiano mkubwa wa kuuzwa nje ya nchi. Kwa mwaka 2010, theluthi moja ya mauzo yote yaliyouzwa nje ya nchi yalitokana na madini peke yake.

Uvumbuzi wa hivi karibuni wa hifadhi ya gesi asilia baharini, na uwezekano wa kupata mafuta, utafanya uchimbaji wa mafuta kuwa muhimu kwa Tanzania. Matarajio yanazidisha uchimbaji, utekelezaji wa mauzo ya nje, na utumiaji wa ndani wa maliasili unachangia kwa kiasi kikubwa uchumi mzuri. Inaweza pia kuchangia katika kutatua matatizo ya nishati yaliyokuwepo kwa muda mrefu, na kwa kiwango kikubwa kuinua mapato ya ndani. Makadirio ya hivi karibuni ni kwamba gesi asilia itakapozalishwa kwa kiwango cha juu, mapato kutokana na uchimbaji peke yake yatakuwa mara tatu zaidi kwa wakati huu (ODA) katika Tanzania. Zaidi ya vipindi vya muda mfupi na wa kati, hata hivyo, mapato kutokana na gesi asilia hayatakuwa dhahiri, na inawezekana kwamba serikali inaweza ikaweka rehani mapato ya baadaye kukidhi mahitaji ya muda mfupi. Hali hii tayari imeonekana kuwa dhahiri kwa serikali kuongeza kukopa.

Uzoefu uliopo sasa kutokana na uchimbaji wa madini, hakuna uhakika kwamba uendelezaji wa gesi asilia utazalisha idadi kubwa ya ajira mpya, labda hatua mahsusi za sera mpya zitachukuliwa kusimamia jambo hili. Serikali ya Tanzania inafahamu faida kubwa ya ukuaji wa maendeleo ya uchumi wa taifa ikiwa kutakuwa na muunganiko wa uchimbaji wa gesi asilia na uchumi wa ndani utaanzishwa, kwa mfano kwa kupitia utekelezaji wa ndani na kuingia mikataba na wengine (subcontracting). Sera za kodi zilizopo zinaangaliwa upya ili ziweze kutumia uzoefu wa kimataifa katika kuhakikisha upatikanaji wa mapato ya taifa yanayotokana na matumizi ya akiba ya gesi. Mwaka 2012, sera za Tanzania katika sekta ya uchimbaji wa madini ilitamka kukubaliana na viwango vya kimataifa vya (EITI) na utekelezaji wa sheria muhimu umeanza.

## 2.8 CHANGAMOTO ZA MAZINGIRA NA MABADILIKO YA HALI YA HEWA

Uchumi wa Tanzania umebakia kutokuwa salama kutokana na mazingira yake. Nchi imetegemea sana nishati ya umeme wa maji kwa ajili ya mahitaji yake ya umeme, lakini katika miaka ya hivi karibuni uzalishaji wa umeme umekuwa hautoshelezi kutokana na ukosefu wa mvua za kutosha pamoja na kupungua kwa kina cha maji katika mabwawa yanayotumika katika uzalishaji wa umeme. Athari za mabadiliko ya hali ya hewa kwa Tanzania pia zimeonekana wazi kwa kilimo kutokana na kutegemea mvua. Sehemu kubwa ya nchi inategemea mvua za misimu kwa ajili ya kilimo, na kuna uhusiano wa karibu kati ya mabadiliko ya kiasi cha mvua inayopatikana na ongezeko la ukuaji wa uchumi wa nchi kwa mwaka. Karibu nusu ya pato la taifa linatokana na kilimo, na upungufu wa uzalishaji katika kilimo umekwishatokea kutokana na mabadiliko ya upatikanaji wa mvua. Katika

baadhi ya mikoa, hali hii imesababisha matatizo ya uzalishaji wa chakula na hifadhi ya chakula. Mwanzoni mwa mwaka 2013, Tanzania kwa mara ya kwanza ilipitisha mpango mkakati wa kupunguza athari za mabadiliko ya hali ya hewa.

## 2.9 USHIRIKIANO WA KIKANDA: NCHI ZA KUSINI MWA AFRIKA (SADC) NA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI (EAC)

Ushirikiano wa kikanda, una jukumu muhimu , kisiasa na kiuchumi, katika suala la kupunguza hatari ya migogoro ya kikanda. Kiuchumi, inahusu masuala ya ushirikiano katika rasilimali na masoko kwa ajili ya kufikia kiwango cha ukuzaji uchumi, pamoja na uwezekano wa kitaalamu na ushindani mkubwa. Kisiasa, Tanzania imejikita zaidi kusini mwa Afrika kwenye Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Africa (SADC), wakati kwa upande wa shughuli za kiuchumi, inajihusisha zaidi na Jumuiya ya Afrika ya Mashariki (EAC) ambayo ilianzinduliwa upya mwaka 2000.

Yapo matumaini kuhusu uwezo wa Tanzania katika kushika nafasi ya uongozi katika utatuzi wa migororo ya kisiasa katika kanda.Tanzania imetuma vikosi vyake vya askari kukabiliana na migogoro katika nchi za Sudani na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, na hii imeonyesha utayari wa nia yake katika kubeba jukumu hilo.

Jumuiya ya Afika Mashariki (EAC) iko makini kufanikisha muungano wa kiuchumi. Ushirikiano uliopo sasa unajumuisha umoja wa forodha na soko la pamoja. Ushirikiano huu utakapotekelezwa kikamilifu, utasaidia kuwepo kwa ushuru wa pamoja na usafirishaji huru wa bidhaa bila vikwazo katika ukanda, na soko la pamoja litawezesha kuundwa kwa soko moja la kanda lenye kuruhusu usafishaji wa bidhaa zinazozalishwa, likijumuisha nguvukazi na mitaji. Mipango inaandaliwa ya kuwa na sarafu ya pamoja, kwa lengo la kuwa na shirikisho kamili kisiasa. Hata hivyo, mkazo mkubwa kwa sasa upo katika ushirikiano wa kiuchumi. Uchumi binafsi katika nchi za Afrika ya Mashariki bado ni mdogo. Jumla ya zao ghafi la taifa (GNP) kwa nchi zote za Afrika ya Mashariki zikijumuishwa pamoja (yaani Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi na Tanzania, zenye wakazi takribani milioni 135) ni robo tu ya Dermark, na zao ghafi la taifa (GNP) la Tanzania ni karibu asilimia saba (7%) ya ile la Denmark, ingawa Tanzania ina idadi ya watu mara nane ya ile ya Denmark. Kuongezeka kwa ushirikiano wa kiuchumi katika ukanda, hivyo unaleta faida kubwa katika ushindani ulioboreshwa na hii itamaanisha kuwa makampuni binafsi yatapata fursa kubwa katika soko la ndani.

Tanzania imechukua mwelekeo wa tahadhari katika mchakato wa ushirikiano, kama ilivyo watanzania wengi wanahitaji muda zaidi wa kujiandaa kinchi kwa ajili ya usafirishaji huru wa bidhaa, nguvukazi na mitaji. Sekta kama uhamiaji na umiliki wa ardhi ni masuala nyeti kwa Tanzania. Mbali ya haya, Tanzania imeendelea mbele na agenda ya mageuzi ya EAC, na hatua za kuridhisha zimekwishafanyika. Hata hivyo, isifikiriwe kwamba Jumuiya ya Afrika Mashariki inaweza kukua bila usawa ikiwa na baadhi ya nchi zinazokwenda haraka kuliko Tanzania katika mchakato wa ushirikiano.

## 2.10 MISAADA YA NJE KWA TANZANIA

Ukuaji wa juu wa uchumi na mapato ya ndani kwa kiasi fulani yanayotokana na kodi, umepunguza kwa kiasi fulani historia ya Tanzania katika utegemezi mkubwa wa misaada kutoka nje. Hata hivyo, misaada imeendelea kugharamia karibu theluthi moja ya matumizi ya umma (yanayofikia karibu asilimia nane (8%) ya pato la taifa). Hili linawezekana kubadilika kwa haraka katika muongo ujao, ambapo uendelezwaji wa ukuaji wa juu wa uchumi na ongezeko la mapato kutokana na gesi asilia unaweza kupunguza umuhimu wa misaada ya maendeleo kwa Tanzania.

Tanzania imekuwa mstari wa mbele kimataifa katika kuimarisha ufanisi katika matumizi ya misaada. Kiashiria kikuu cha juhudi hizi ilikuwa ni hatua iliyoiwezesha serikali kupata msaada wa bajeti kwa ujumla (General Budget Support) kuanzia mwaka 2000. Gawio la msaada wa bajeti kuu (GBS) katika misaada halijaongezeka kama ilivyotarajiwa, zaidi ya theluthi mbili

ya taarifa yote ya ODA iliyotolewa katika mifumo wa serikali kupitia njia mbalimbali, na theluthi moja inayobaki ni kwa ajili ya bajeti ya msaada wa bajeti kuu (GBS). Kwa ujumla msaada wa ODA kwa Tanzania umeendelea kuongezeka kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita, uwiano kati ya gawio umebadilika, ambapo gawio la msaada wa bajeti kuu (GBS) linapungua kiasi, mfuko umebakia kuwa imara na misaada ya kusaidia miradi unaongezeka.

Takwimu za matokeo ya misaada ya maendeleo kwa Tanzania zinaonyesha kuna mafanikio katika maeneo ambayo rasilimali zilielekezwa. Hii inathibitika hasa katika sekta za kijamii, wakati misaada kutoka nje ya nchi pia imeisaidia serikali kuweka vipaumbele vya matumizi ya rasilimali zake. Na ambapo misaada ya kusadia juhudi za jumla imechangia katika uboreshaji wa sekta zinazohudumiwa na mfuko wa maendeleo kuelekea malengo ya milenia (MDG). Misaada, hasa katika mfumo wa msaada wa bajeti kuu (GBS) na utaratibu wa mfuko (basket modalities), umesababisha uhitaji na pia umechangia kuboresha mifumo ya kitaifa ya fedha na usimamizi thabiti na uwajibikaji katika utawala wa umma.

## 2.11 USHINIKIZAJI NA KASI YA MAGEUZI

Kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo, Tanzania imekuwa ikitekeleza mageuzi ya msingi katika uchumi na sekta za umma kwa miaka mingi. Baada ya kupata matokeo mazuri katika miaka ya mwanzoni, mabadiliko mengi ya msingi yamedumaa katika miaka ya karibuni. Hii inaweza kuelezwa kutokana na ukweli kwamba mageuzi ya kizazi cha awamu ya pili ni magumu zaidi kutekelezwa, na kwamba uwezo wa mifumo unabaki kuwa finyu. Hata hivyo, kuna kiwango fulani pia cha ugumu wa mageuzi ndani ya vyombo vya serikali. Kwa kutambua kwamba utekelezaji hafifu wa mageuzi ni sababu mojawapo ya kikwazo kikubwa katika jitihada za nchi za kufikia malengo ya maendeleo. Hivi karibuni, serikali ya Tanzania imeiga mkakati unaoitwa “Matokeo Makubwa Sasa” (BRN) ili kuharakisha utekelezaji katika sekta zilizochaguliwa na zenye mikakati muhimu.

Wazo la mkakati wa BRN limetoka Malaysia, na linatekelezwa kwa muundo wa kutoka juu kwenda chini likisimamiwa na Rais. Lengo ni kufikia mpangilio sahihi wa vipaumbele vya sera kwa matendo na kuunganishwa na mikakati ya ugawaji wa rasilimali kwa sekta zilizopewa kipaumbele, na mtazamo dhabiti katika utekelezaji na ufuatiliaji wa matokeo. Sekta sita zimechaguliwa na kupewa kipaumbele kama mzunguko wa kwanza kwa ajili ya matokeo ya awali: nishati na uzalishaji wa umeme, uchukuzi, kilimo, elimu, maji na uhamasishaji rasilimali. Inatarajiwa kwamba mzunguko unaofuata utajumuisha sekta ya afya. Maamuzi kuhusu utaratibu mpya wa utekelezaji wa mchakato wa mageuzi ni mpya sana, lakini inawezekana kwamba kutumia mbinu ya BRN kutaleta mabadiliko ya kweli na matokeo chanya, hasa ikiwa serikali itafanikiwa katika kuanzisha usimamizi thabiti katika kuunda mfumo imara wa kitaasisi utakao hakikisha usimamizi, udhibiti na kwamba sekta za umma zitatoa matokeo ya kweli yaliyopangwa.

# 3. MALENGO MKAKATI YA JUMLA NA MAENEO LENGWA YA DENMARK KATIKA USHIRIKIANO

Ushirikiano wa Denmark na Tanzania unachukua hatua yake ya kuondokana na siasa, uchumi na changamoto za kijamii kama zilivyoelezwa hapo juu. Ushirikiano unajengwa kwa Denmark kujitolea kwa dhati kuisaidia Tanzania kukabiliana na changamoto hizi na kusaidia kutumia fursa nyingi zilizopo. Denmark inasaidia dira ya maendeleo ya 2025 ya serikali ya Tanzania na mipango yake ya maendeleo ya kitaifa, ikijumuisha mbinu za ukuaji za kitaifa na kupunguza umasikini (MKUKUTA II 2010-2015) na taswira ya mpango wa muda mrefu (2011-2025) na mfululizo wa utekelezaji wa mpango wa maendeleo wa miaka mitano. Inafikiriwa kwamba mpango wa Matokeo Makubwa Sasa (BRN) utaimarisha utekelezaji wa mikakati hii.

Kwa jumla malengo mkakati ya ushirikiano ya Denmark na Tanzania ni:

1. Kupunguza umaskini na ukosekanaji wa usawa na kuhakikisha upatikanaji mzuri wa huduma bora za kijamii, hususani katika sekta ya afya.
2. Kusaidia kwa pamoja ukuaji uchumi wa kijani na ajira.
3. Kuimarisha demokrasia, utawala bora na utawala wa sheria na kuheshimu haki zote za binadamu.

Tofauti hizi za malengo mkakati zinahusiana kwa karibu. Amani, utulivu na demokrasia vimekuwa vielelezo muhimu vya maendeleo chanya kwa Tanzania. Kuendelea kuwepo kwa amani na kukua kwa demokrasia, maboresho ya haki za binadamu, utawala wa sheria na utawala vitakuwa muhimu kwa uchumi wa baadaye na maendeleo ya kijamii pamoja na kuboresha mazingira ya biashara kwa kuhakikisha usawa zaidi na haki katika kutoa huduma za kijamii. Kuongezeka kwa ushirikiano wa kibiashara na nchi jirani pamoja na nchi nyingine za kigeni kutasaidia kukua kiuchumi na kuongeza zaidi nafasi za ajira. Pamoja na ukuaji na fursa nzuri za ajira hasa katika maeneo ya vijijini ni msingi muhimu wa kupunguza umaskini na kuboresha hali ya ustawi wa jamii, lakini pia, kuimarisha utulivu na kuendelea kuwepo kwa historia ya mshikamano wa amani kati ya makundi tofauti ya kijamii na kikabila kwa Tanzania.

Ili kufikia malengo haya, maeneo lengwa yafuatayo yamechaguliwa kwa ushirikiano:

a. Sekta ya afya;
b. Sekta ya kilimo;
c. Utawala bora na upatikanaji wa Haki
d. Amani katika ukanda na utulivu.


Maeneo haya ya msingi yamechaguliwa kutegemeana na uchambuzi wa changamoto muhimu na mahitaji yaliyoelezwa hapo awali katika rasimu hii ya sera ya nchi. Katika masuala ya fedha, msaada wa maendeleo wa Denmark ni kiasi cha asilimia sifuri nukta tatu (0.3%) ya pato la taifa la Tanzania na karibu asilimia moja (1%) tu ya jumla ya bajeti yote ya umma. Vipaumbele vya juhudi za Denmark, vinategemea kimsingi tathmini ambayo Denmark imeweza kuwa kichocheo cha kuvutia washirika wengine, sekta binafsi na za umma kwa pamoja, kuelekea malengo ya jumla ya maendeleo ya Tanzania. Aidha, Denmark inatazamia kuendelea kwa ushirikiano ambao utategemea uimara, ujuzi wa muda mrefu na uwezo wa nafasi Denmark iliyopata kwa miaka mingi ya ushirikiano katika maeneo hayo.

Denmark itafanya kazi na wabia, watendaji kwa ukaribu na upana mkubwa na kwa kiasi kwamba wako tayari kuchangia na kuhakikisha uhitaji wa mabadiliko na mageuzi. Hii inamaanisha kwanza kabisa kwa serikali ya Tanzania, lakini vile vile kwa bunge, asasi za kiraia, vyombo vya habari na sekta binafsi. Zaidi ya nusu ya mfuko wa fedha wa Denmark unatarajiwa kuelekezwa moja kwa moja kupitia mifumo ya serikali, hasa kwa kuunga mkono upunguzaji wa umaskini na kuhakikisha usambazaji endelevu wa huduma za kijamii.

Serikali ya Denmark imechukua mtazamo sahihi wa maendeleo, ikimaanisha kwamba Denmark itatumia utaratibu wa kushughulikia kanuni za misingi ya haki za binadamu bila ubaguzi, umuhimu wa ushiriki, uwazi na uchumi na uwajibikaji wa kisiasa katika maeneo yote ambayo Denmark na Tanzania wanashirikiana.

Ushirikiano wa maendeleo utasimamiwa na kanuni za kimataifa kwa ufanisi wa misaada. Hii inajumuisha kanuni za umiliki, mfungamano, upatanisho, matokeo- elekezi na uwajibikaji wa kiuchumi kwa pamoja. Kwa kiasi kikubwa sana Denmark, itasaidia mikakati ya maendeleo ya kitaifa na kufanya kazi kupitia mifumo ya kitaifa.

Ushirikiano na Tanzania unaainishwa kwa kina na utamaduni uliokuzwa vizuri




kwa mazungumzo na uratibu. Denmark itaendelea kushiriki kikamilifu katika mjadala wa sera na Tanzania, kimsingi pande zote mbili kwa kupitia utaratibu ulio imara wa mazungumzo na serikali pamoja na wadau wa maendeleo. Kwa sasa Tanzania ina wadau wa maendeleo 40, wadau wakubwa sana ni Marekani, Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika, Umoja wa Nchi za Ulaya, Uingereza /DFID na nchi za Nordic. Denmark imejikita katika mazungumzo yanayoendelea, ushirikiano, na uratibu wa wadau hawa muhimu wa maendeleo, ikijumuisha programu za pamoja katika mfuko wa fedha na katika kundi la wafadhili wa kusaidia bajeti kuu (GBS).

Denmark inashirikiana kwa karibu na ujumbe wa Jumuiya ya Ulaya (EU) na wanachama wa nchi nyingine za Umoja wa Ulaya (EU), na wakati fursa inapotokea, itaendelea kutafuta wigo wa kuimarisha ushirikiano huu. Katikaupendeleo huu wa pekee ni ushirikiano dhabiti na upatanisho wa nyenzo za misaada mbalimbali kwa kusaidia bajeti kuu (GBS), Denmark pamoja na Jumuiya ya Ulaya tayari kwa sehemu kubwa wamefungamanisha taratibu zao. Katika Brussels pia, Denmark itashiriki kwa kikamulifu katika kuendeleza sera za Jumuiya ya Ulaya zinazohusu Tanzania.

Denmark itaongeza msaada na kukuza ushirikiano wa kibiashara na Tanzania, pia katika muktadha wa kuongeza muungano wa kiuchumi katika kanda ya Afrika Mashariki. Denmark itaongeza ushirikiano wake na Tanzania katika masuala ya kimataifa yanayohusu nchi zote mbili, kama vile kudumisha amani katika ukanda, vita dhidi ya uharamia, kuimarisha ajenda ya kimataifa ya haki za binadamu, utawala wa sheria na sera za biashara zilizoboreshwa. Denmark pia itafanya kazi ya kuimarisha ushirikiano katika nyanja za ubadilishanaji wa utamaduni na Tanzania.

Hivyo, ushiriki wa Denmark katika Tanzania unachukuwa mtazamo wa muundo unganishi ambao viashiria vya mtu binafsi - programu za kimaendeleo- ushiriki wa kibiashara na majukwaa ya kisiasa na pande zote mbili zinazoimarishana ili kuhakikisha matokeo na ufanisi wa hali ya juu. Nyenzo zote zitakazopatikana zitazingatiwa katika kufikia mikakati malengo na zitatumika katika maeneo husika kwa ushirikiano wa baadaye kama ilivyoainishwa katika aya zifuatazo.

## 3.1 KUPUNGUZA UMASKINI, FURSA SAWA NA KUHAKIKISHA UPATIKANAJI WA HUDUMA BORA ZA JAMII, HUSUSANI KATIKA SEKTA YA AFYA

Msaada wa Denmark kwa ajili ya kukuza haki za Watanzania maskini kuwa na maisha bora utalenga kukuza haki za binadamu kwa Watanzania pamoja na kukuza njia ambazo ukuaji wa uchumi unaanzishwa na kusambazwa Tanzania. Kitovu kitakuwa katika maeneo matatu; ajira, huduma za jamii na athari za mgawanyo wa mapato kupitia mfumo wa kodi.

Uundaji na utekelezaji wa sera za kusaidia umaskini na ambazo ni bora na za usawa zaidi katika usambazaji wa huduma za jamii ni wajibu wa kwanza na muhimu na ni wa lazima kwa serikali ya Tanzania. Serikali ya Tanzania iliahidi yenyewe uhakika wa kutimiza wajibu huu,na Denmark itaisaidia serikali katika jitihada zake. Ushirikiano wa Tanzania na Denmark utatilia mkazo utawala bora ikiwemo utoaji na upatikanaji wa huduma bora edelevu za jamii, na maendeleo salama yenye faida kwa Watanzania wote, hususani maeneo ya vijijini, pamoja na maeneo yanayokaliwa na wenyeji.

Denmark inaisaidia Tanzania katika malengo yake ya muda mrefu kuweza kuwa nchi ya kipato cha kati ifikapo mwaka 2025 (Dira 2025). Lengo hili limedhamiria umaskini uliokithiri kuondolewa kabisa. Katika kipindi kifupi, malengo ya serikali ni kupunguza kipato cha umaskini kwa asilimia ishirini na nne (24%) ifikapo mwaka 2015 (lengo la MMM ni asilimia kumi na tisa (19%). Serikali inataka kupunguza kipato cha umaskini kwa ukuaji wa ajira na maendeleo. Zaidi sana, malengo ya serikali ni kuanzisha na kuhakikisha heshima na ajira bora hususan kwa wanawake, vijana na walemavu na kupunguza idadi ya wasiokuwa na ajira hadi kufikia asilimia tano (5%). Hili litasababisha kuanzishwa kwa zaidi ya nafasi milioni tatu za ajira kwa kipindi cha miaka mitano ijayo. Juhudi ni kuboresha uzalishaji katika sekta ya kilimo na kipengele hiki ni cha muhimu sana kwa muktadha huu, na mpango wa serikali ni kuongeza ukuaji wa kilimo hadi ailimia sita (6%) ifikapo mwaka 2015.

Kwa kuongezea katika mpango wa moja kwa moja wa kupunguza umaskini, serikali inapanga kuboresha utoaji wa huduma za jamii kwa kiwango kikubwa na kwa mapana. Dira na mpango wa 2025 umelenga elimu ya msingi kwa wote, kutokomeza ujinga na kuwepo kwa mafunzo ya elimu ya juu na kuwapa ujuzi Watanzania ili nchi iweze kufikia upeo mkubwa wa mahitaji ya kibinadamu na nafasi ya kuweza kutatua changamoto kubwa za maendeleo zinazoikabili nchi.

Katika sekta ya afya, malengo ni kuhakikisha upatikanaji na ubora wa afya ya msingi hususan huduma bora kwa wote hasa upatikanaji wa huduma ya afya ya uzazi (ikiwepo na ya uzazi wa mpango) kwa wote wenye uhitaji. Lengo likiwa ni kupunguza vifo vya watoto wachanga, watoto pamoja na viwango vya wajawazito kwa robo moja ya kiwango kilichopo sasa.

Zaidi ya wastani, serikali imelenga kuhakikisha watoto wote kuanzia utotoni, watapatiwa huduma ya elimu bure, na kuwepo fursa kwa shule za msingi na sekondari kwa wavulana na wasichana. Malengo haya yatajumuisha uandikishaji wototo wa shule ya awali na msingi kwa kiasi cha kufikia asilimia mia moja (100%), na kuwepo kwa idadi ya kutosha ya walimu waliofunzwa, ili kuwepo na mwalimu mmoja kwa wanafunzi 45 kwa shule za msingi, na mwalimu mmoja kwa wanafunzi 25 kwa shule za sekondari.

Katika sekta ya afya, serikali ina lengo la kuboresha viwango vya maisha, afya, lishe na ustawi, hasa kwa watoto, wanawake na makundi hasa yaliyopo katika mazingira magumu. Denmark itaisaidia serikali katika jitihada zake za kuongeza kasi ya utoaji wa huduma bora za afya ya msingi kwa wote kufikia mwaka 2017 na kukaratabati na kuboresha miundombinu ya zamani na kuanzisha nyingine mpya ili kuhakikisha uwezekano mkubwa wa usawa na fursa sawa ya huduma bora ya afya kwa Watanzania wote.

Malengo ya maendeleo ya serikali ni yenye nia na gharama. Mpango wa serikali ni kuongeza mapato ya serikali kwa zaidi ya asilimia themanini (80%) kwa kipindi cha miaka mitano ijayo, na Denmark itaisaidia Mamlaka ya Mapato ya Tanzania kufikia malengo ya matarajio haya. Hili linaenda sambamba na kuongeza ukusanyaji wa mapato ya serikali, kimsingi kupitia kodi kutoka asilimia kumi na nane (18%) hadi asilimia ishirini na mbili (22%) ya pato la taifa (GDP). Kama serikali itafikia lengo lake, kuongezeka kwa kodi kila mwaka na leseni ya mapato peke yake katika mwaka 2018 italingana mara 25 zaidi ya msaada wa Denmark ODA kwa Tanzania. Denmark itaunga mkono mipango inayoboresha

usimamizi wa fedha za umma, ikijumuisha usimamizi wa mapato ya Taifa. Juhudi hizi zitakuwa muhimu kwa kuhakikisha uwajibikaji wa uongozi uliosambamba na na msaada wa bajeti ya kuu , kupunguza madhara yanayoambatana na mfumo huo wa msaada. Denmark itaendelea kusisitiza uimarishaji wa kuheshimu utawala wa sheria na aina zote za haki za binadamu. Denmark italenga zaidi hasa katika uwazi na uwajibikaji katika utawala na kupambana dhidi ya nyanja zote za rushwa.

Ushirikiano na Serikali ya Tanzania itasimamia katika msingi wa mapatano ya maendeleo na mkataba kati ya serikali hizi mbili, ambapo Denmark ilielekeza mfuko wake wa fedha katika bajeti ya taifa kwa kutegemea uaminifu wa serikali ya Tanzania katika kanuni za uongozi bora na uendelezaji wa haki za binadamu na demokrasia, pamoja na mafanikio ya malengo maalum ya maendeleo lengwa mwaka kwa mwaka. Kanuni hii ina lengo la kuhakikisha:

- Kuongeza ufanisi katika misaada na umiliki wa nchi, gharama ndogo katika usimamizi wa misaada ya maendeleo, matarajio makubwa yanayotokana na mtiririko wa misaada, ikitiliwa mkazo usimamizi wa fedha na matumizi ya fedha za umma, kuimarisha mipango ya kitaifa na mchakato wa bajeti pamoja na uwajibikaji wa kifedha uliotolewa na wafadhili kwa Watanzania wote.

- Kuboresha mfumo wa ufuatiliaji na tathmini na kuhakikisha uwepo wa wajibu wa kusimamia misaada:

- Kuimarisha utumiaji wa mipango ya kitaifa na mchakato wa bajeti na kuimarisha uwezo wa Mamlaka za Serikali za Mitaa, kwa sababu ziko mstari wa mbele katika utekelezaji wa mikakati ya kupunguza maskini.

Mtazamo wa haki za binadamu unataka ufanyike kwa njia ya mazungumzo na misaada ya kiufundi ambapo Denmark itazingatia:

- Kuanzisha kwa pamoja uchumi wenye nguvu na taasisi za kisiasa kuweza kutimiza majukumu yao kama wenye dhamana.

- Urejeshwaji wa rasilimali katika jamii ili zitumike kama nyongeza ya faida kwa maskini na vikundi vilivyo katika mazingira magumu. Hii inahusu uhalisi wa rasilimali za kiuchumi pamoja na bidhaa za kiraia kama vile miundombinu, nishati, afya na elimu.

- Uhitaji wa ukuaji ili uwe endelevu kwa pamoja, hasa kuongeza ajira katika maeneo ya vijijini.

Denmark pia itashiriki katika mazungumzo na serikali ya Tanzania juu ya masuala yanayohusiana na matumizi ya umma. Hii inajumuisha sekta za kijamii, hasa afya, kupewa kipaumbele katika bajeti ya taifa. Sera ya mgawanyo wa mapato kwa kutekeleza haki za kiraia, kisiasa, kiuchumi, kijamii na haki za tamaduni pia ni mada itakayotiliwa mkazo katika majukwaa ya mazungumzo ya Denmark – Tanzania.

Denmark itasisitiza kwamba msaada utalenga katika matokeo dhahiri, katika kutimiza kwa ujumla upungazaji wa umaskini na kukamilisha malengo ya maendeleo yaliyowekwa na Serikali ya Tanzania, kama vile makubaliano ya malengo mahususi kati ya serikali na wadau wake wa maendeleo. Mtazamo wa matokeo ya kudumu ni muhimu ili kuhakikisha watakofaidika kwanza na msaada wa Denmark katika mfumo wa bajeti kuu (GBS) watakuwa watu maskini Tanzania, na hii ina maana kwamba sehemu ya bajeti inayozingatiwa itasitishwa kama makubaliano ya malengo hayatafikiwa.

***Mtandao wa Usalama na Hifadhi ya Jamii***
Usawa katika utoaji wa huduma za kijamii ni sharti la awali la utekelezaji sahihi wa mtandao mpana wa usalama wa jamii. Juhudi za kitaifa kwa sasa zinalenga katika kuongeza huduma ya mfuko wa bima ya afya katika ngazi ya kitaifa na jumuiya na kupunguza utaratibu wa malipo kwa familia zenye kipato cha chini kama ikizingatiwa, kwa mfano chanjo ya watoto, elimu kwa watoto wa kike na mengine kama hayo. Denmark kupitia mazungumzo ya pamoja ya mfuko wa bajeti kuu (GBS) na sekta ya afya, itachangia katika kuhakikisha kwamba maskini, wataweza kupatiwa huduma zilizopo katika mipango ya sekta za umma na binafsi kwa pamoja, uzoefu uliohakikiwa wa kuweza kupata huduma bora za jamii.

**3.1.1 Eneo Lengwa**
**Msaada kwa Sekta ya Afya**

Sehemu ya mchango wa Denmark kwa bajeti ya Tanzania italenga hasa kusaidia sekta ya afya. Lengo ni kuboresha afya na ustawi katika makundi maskini ya jamii ya Tanzania kwa kuimarisha uwezo wa mifumo ya kitaifa (ikiwa ni pamoja na wenyeji) kuhakikisha fursa sawa na bora za huduma ya afya kwa wote. Hii ni pamoja na kudumisha na kuendeleza zaidi mafanikio ya matokeo kulingana na malengo ya milenia ya Umoja wa Mataifa. Mkazo zaidi utatolewa hasa kwenye masuala ya usawa na ubora.

Mafanikio ya malengo ya ujumla yatafikiwa kwa kuzingatia:

- Msaada wa pamoja katika mfumo wa afya, pamoja na kukuza mfumo wa pamoja wa kuratibu matokeo ya msingi ya usimamizi wa fedha kulingana na mikakati ya kitaifa na kisekta.

- Ushirikiano wa wadau binafsi na wa umma katika kuunga mkono ubunifu wa utaratibu wa kufadhili na njia za kutoa huduma za afya, wakati huo huo wakiongeza jukumu la utoaji huduma za afya kwa sekta binafsi.

- Kuimarisha juhudi kwa ajili ya afya ya uzazi, ikiwa ni pamoja na kuunga mkono haki za kujamiana na uzazi.

- Denmark itaendeleza utekelezaji wa haki za msingi katika utoaji wa aina zote za misaada katika sekta ya afya.

Kutokana na lengo la kusaidia sekta ya afya, Denmark inaweza kutumia uzoefu wake wa muda mrefu katika sekta hii katika Tanzania kwa kuimarisha na kuunganisha huduma za afya zilizopo, kama mipango itatekelezwa kama ilivyotarajiwa, kwa sababu ni sekta iliyopewa kipaumbele katika mpango Mkakati wa Tekeleza Sasa kwa matokeo makubwa. Kama afya ikiwa sehemu ya mkakati huo itaipa kipaumbele sekta hii uwezo muhimu wa kuongezeka. Denmark itaendesha mafunzo ya jinsi sekta ya afya inafadhiliwa ili kuhakikisha kuwa mifuko ya fedha inatumika kwa ufanisi iwezekanavyo, pia katika mtazamo huu, Zanzibar kipekee, itawezekana hapo baadaye kupewa misaada katika sekta ya afya na itatathminiwa wakati wa upitiaji wa katiba iliyopo kukamilika.

Ili kushughulikia tofauti muhimu katika suala la upatikanaji wa huduma bora za afya kama zinavyoathiri makundi mbalimbali katika jamii, Denmark italenga upande wa ugavi na upande wa mahitaji. Hii ni pamoja na kuhakikisha juhudi za ugawaji sawa na wazi wa rasilimali katika ngazi ya wilaya. Itakuwa muhimu kuhakikisha kwamba huduma za msingi za afya zinakubalika katika kiwango kinachokubalika, pia zinapatikana kwa wakati kwa watu wote na mahali pote na zinatolewa hivyo kwamba ni uchumi endelevu wa muda mrefu. Denmark itajikita katika rasilimali zinazokwenda ngazi ya wilaya (kutoka asilimia hamsini (50%) mpaka asilimia sabini na tano(75%) ya misaada yote katika sekta); kuhakikisha ugawaji sawa na usambazaji wa michango ya kifedha kwa rasilimali za afya; na kuhakikisha usawa zaidi katika mgawanyo wa wataalamu wa afya kwa wilaya zote.

Juhudi hizi zitakuzwa kupitia mazungumzo ya sera yanayohusiana na mfuko wa bajeti kuu (GBS). Juhudi za kukuza usawa na ubora wa utoaji wa huduma za afya zinahitaji uhusiano wa karibu wa msaada mkubwa wa Denmark kwa uongozi bora na haki za binadamu.

Uhakika wa huduma za msingi za afya kimsingi ni jukumu la serikali. Hata hivyo, serikali haitoi huduma za afya yenyewe. Taasisi na mashirika binafsi yanatoa kiasi cha asilimia arobaini (40%) cha huduma yote inayotolewa kwa sasa, na kujihusisha kwa taasisi hizi ni katika msingi wa imani ya mashirika yanayotegemea na yasiyotegemea faida. Taasisi za binafsi pia zinatoa huduma ya afya kwa uwiano mkubwa kwa sehemu za maeneo ya vijijini na baadhi ya makundi ya watu maskini. Kwa hiyo, Denmark italenga kutoa msaada kwa ushirikiano uliopo kati ya serikali na wadau binafsi kwa nia ya kuchochea na kuimarisha misaada kwa ushiriki wa sekta binafsi katika kujihusisha kukuza fursa, upatikanaji na ubora katika huduma ya afya.

Licha ya kuwasaidia wadau binafsi wa serikali katika maeneo ya mijini, Denmark itasaidia kuimarisha baraza la ushirikiano la serikali na wadau binafsi kwa ngazi ya mikoa (jumla ya mikoa 25). Itaimarisha ushikiano uliopo kati ya sekta za serikali na binafsi katika kutafuta kuhakikisha kuongeza fursa na uchaguzi kwa watumiaji wa afya na huduma za jamii.

## PROGRAMU YA DENMARK KUCHANGIA MALENGO YA KITAIFA YA TANZANIA KUHUSIANA NA:

1. Kupunguza ongezeko la watu kutoka 2.9% kwa mwaka (2002) mpaka 2.7% kwa mwaka katika mwaka 2015.
2. Kupunguza uwiano wa vifo vya akina mama wajawazito kutoka 454 kwa kila watoto hai 100,000 (2010) mpaka 265 kwa kila watoto hai 100,000 ifikapo mwaka 2015.
3. Ongezeko la idadi ya watoto wanaozaliwa kwa kuhudumiwa na wafanyakazi wa afya wenye ujuzi kutoka 50.6% (2010) hadi 80% (2015).
4. Kushuka kwa kiwango cha uzazi kutoka 5.4 (2010) na 5 ifikapo mwaka 2015.
5. Kupunguza uwiano wa wilaya zenye wauguzi / wakunga wachache zaidi ya 3 kwa kila idadi ya watu 10,000 kutoka 55% (2012) mpaka 34% (2015).

## 3.2 KUKUZA UCHUMI WA KIJANI NA AJIRA

Lengo la Denmark kusaidia ni kuimarisha ajira na fursa ya kipato kwa wanawake na wanaume katika uchumi wa kijani, ikiwa ni pamoja na ukuaji wa biashara ndogo ndogo na za kati (MSMEs). Hili ni eneo ambalo serikali ya Tanzania ina sera za ushawishi, lakini ni matokeo ya wastani tu yameonekana. Ili kuisaidia Tanzania kufikia  matokeo yanayotarajiwa katika masuala yote ya kazi na kupunguza umaskini, Denmark italenga kusaidia mashirika yasio ya kiserekali, ambayo yana matakwa ya kuongeza kukua kwa uchumi, na katika serikali za mitaa ,ambazo ni washiriki muhimu zaidi wa serikali kwa biashara nchini. Msaada utatolewa sambamba na ufanisi wa utetezi wa kazi za sekta binafsi kwa kuboresha mazingira ya biashara.Tayari kumekuwepo na kiasi kizuri cha mafanikio katika kuendeleza mfumo wa utoaji wa mikopo wa kifedha na mifano ambayo inayoweza kujenga aina ya usalama ili kuwezesha upatikanaji bora wa mikopo katika sekta binafsi. Kazi hii itaendelea na kwa kupanuka.

### 3.2.1 Eneo Lengwa
**Kusaidia Sekta ya Kilimo**

Msaada wa Denmark utashughulikia baadhi ya sababu kubwa zitakazoweza kuchochea ukuaji wa sekta binafsi na ubunifu wa ajira, na mkazo utatiliwa katika kuinua uzalishaji wa mazao ya kilimo. Uchanganuzi wa kina umebainisha idadi ya vikwazo vinavyozuia kukua, ikiwa ni pamoja na ukosekanaji wa masoko, wa fedha na ujuzi. Mtazamo utakuwa katika uanzishaji wa ushirikiano wa wafadhili ili kuendeleza utekelezaji wa maendeleo wenye mtindo unaoweza kubadilika kulingana na mahitaji na utakaoweza kujumuisha wadau wakubwa wa serikali na binafsi. Shughuli zote zitaanzishwa kwa lengo la kumwezesha kila Mtanzania kupata ajira yenye heshima itakayomhakikishia kipato cha wastani cha maisha na uwezekano wa kuisaidia familia. Shughuli hizi zitajikita karibu na wale waliothamini uzalishaji unaohusiana na kilimo, ambao una uwezo mkubwa. Kutakuwepo na mtazamo madhubuti wa ukuaji wa uchumi wa kijani, hasa pale penye kuahidi uwezekano wa kuanzisha ajira halali na yenye kipato halali, kwa maskini walio katika maeneo ya vijijini na miji midogo, bila kuwasahau wanawake na vijana. Juhudi zitalenga muundo wa vizuizi vya ukuaji, na kujumuisha juhudi zinazolenga katika kuendeleza ujuzi

Juhudi za msaada zinatarajiwa kuwa na matokeo yafuatayo:

- Kuongezeka kwa kipato na uzalishaji zaidi hasa kwa wakulima wadogo wadogo maskini. Kuongezeka kwa ajira za muda mfupi, au za kudumu, hasa katika maeneo ya vijijini; muda wa ajira kamili, hasa katika maeneo ya vijijini;
- Ujuzi mkubwa na wa aina mbalimbali pamoja na uwezekano wa kujiajiri miongoni mwa Watanzania waliobahatika kupata elimu na mafunzo. Kuzidisha ushindani na kupata masoko ya biashara ndogo ndogo na za kati (MSMEs).
- Kuboresha hali ya kibiashara, hasa katika kuboresha uwezo wa serikali za mitaa na uwezo wa kutekeleza mabadiliko ya mifumo ya sheria na taratibu.
- Kuboresha upya upatikanaji wa mikopo, kubuni na kuanzisha mfumo wa kifedha, hasa katika maeneo ya vijijini.Lengo la kusaidia katika mfumo wa ajira ni kuwezesha uanzishwaji unaoendana na ajira mpya za kudumu angalau ajira 50,000. Katika utekelezaji, itakuwa sambamba na uanzishaji wa zaidi ya ajira 150,000 za mkataba, au kazi za msimu katika mfululizo wa misaada kupitia mipango. Kwa ujumla, lengo la kusaidia ni kwamba watu zaidi ya milioni moja waweze kufaidika na msaada kwa namna moja au nyingine.

Mtazamo wa haki za msingi wa Denmark unahakikisha kwamba kuna mtazamo wa haki katika makubaliano yote muhimu. Kulingana na haki za binadamu, taasisi za wadau zitafanyiwa tathmini, na wadau watahimizwa kuanzisha na kuchapisha sera zao za haki za binadamu. Ufuatiliaji utatathminiwa. Katika kilimo, msisitizo maalumu utawekwa katika utumiaji wa ardhi na maji kwa vikundi tofauti (wakiwemo wafugaji). Kuingilia kati thamani tofauti tofauti kwa kuzingatia uchambuzi wa ukuaji wa uchumi wa kijani na utafiti wa jinsia. Mikakati ya Tanzania ya kupunguza makali ya matokeo ya mabadiliko ya hali ya hewa itajumuishwa kuwa sehemu ya msingi.

Denmark pia itaendelea kusaidia mchakato wa uchumi wa ushirikiano wa kikanda katika Afrika Mashariki kwa msaada wa moja kwa moja kwa Shirika la Uchumi la Afrika Mashariki na Chapa ya Afrika ya Mashariki, lengo likiwa ni kuboresha ufanisi wa usafiri katika eneo la Afrika ya Mashariki na kupunguza gharama za utawala ili biashara katika kanda iweze kuongezeka na kuboresha ushindani. Malengo ya jumla ya msaada kwa kanda ni kupunguza umaskini kupitia uchumi wa kijani na kuongeza ajira. Nchi zote za Afrika Mashariki, ikiwemo Tanzania, zipo kufaidika kwa uchumi imara wa muunganiko wa kikanda na idadi ya ahadi zimekwisha kufanyika kuifanya Afrika Mashariki kuwa na soko moja na umoja wa forodha. Soko la pamoja na umoja wa forodha ni muhimili wa ushirikiano wa Afrika ya Mashariki.

Denmark itatumia uwezo wa kushawishi uwezekano wote wa nyenzo za kimataifa na zana ili kusaidia kukuza uchumi wa kijani na ajira Tanzania, ikiwamo Fedha za Biashara za Shirika la Maendeleo la Denmark (Danida Business Finance), Wadau wa Biashara wa Shirika la Maendeleo la Denmark (Danida Business Partnerships), Mfuko wa Uwekezaji wa Hali ya Hewa (Danida Climate Investment Fund) na Mfuko wa Uwekezaji wa Nchi Zinazoendelea (Investment Fund for Developing Countries) na Baraza la Wakala wa Mauzo ya Nje la Denmark (Denmark's Export Credit Agency na Trade Council).

Tanzania inaendelea kutumia ukopaji nafuu kwa ajili ya mahitaji yake na hii inaweza kuwa faida kubwa kwa kutumia aina mbalimbali za ukopaji wenye masharti nafuu na riba nafuu wa Denmark. Fursa pia zitakuwepo katika sekta zingine tofauti na kilimo, kama kuendeleza upya nishati, uchukuzi na miundombinu, usimamizi wa taka, ubunifu wa viwanda, afya na uzalishaji wa chakula. Wakati huo huo, aina ya mikopo hii itawavutia wawekezaji wa mashirika ya Denmark kwa Tanzania na itaweza kuanzisha ajira na ukuaji endelevu, hasa kwa Tanzania, lakini, pia kwa kiasi fulani Denmark.

**3.2.2 Muunganiko Kati ya Ushirikiano wa Kimaendeleo na Shughuli za Kibiashara**

Ili kuongeza juhudi zilizofanyika katika shughuli za kibiashara katika kusaidia uendelezaji wa kilimo kwanza na ajira, Denmark itaimarisha uchangiaji kati ya shughuli zake za ushirikiano wa kimaendeleo na kibiashara. Mtazamo utakuwa katika kilimo, japo hautakuwa kwenye kilimo tu.

Ushirikiano halisi wa kibiashara kati ya Denmark na Tanzania kwa sasa ni mdogo, na biashara zenye masharti halisi ya kibiashara ni dhahiri hazipo. Biashara za bidhaa za nje kutoka Denmark kwa Tanzania zinahesabika kuwa asilimia sifuri nukta sifuri moja (0.01%) ya jumla ya mauzo ya nje ya Denmark (sawa na DKK milioni 57 – DDK ya mwaka 2011). Hata hivyo, kuna biashara za nje zaidi, ndani ya muundo wa huduma za usafirishaji wa majini na aina nyingine za usafirishaji. Pia kuna mifano midogo ya ushirikiano wa kibiashara kupitia wadau wa kibiashara wa Shirika la Maendeleo la Denmark (DBP), ambayo inaendeleza teknolojia na kuhamisha maarifa kutoka Denmark kwenda katika makampuni ya Tanzania. Denmark imeweka malengo ya kuanzisha miradi ipatayo 20-25 kwa kipindi cha miaka ijayo kupitia wadau wa biashara wa Shirika la Maendeleo la Denmark. Mtazamo utakuwa katika kuimarisha ushindani, kushirikisha majukumu ya kijamii (CSR) na uchumi wa kijani katika Tanzania. Wadau wa biashara wa Shirika la Maendeleo la Denmark wanatarajia kuongeza mauzo katika kuchagua kilimo chenye mfululizo wa thamani na kuongeza ajira mpya kati ya 400-500 kwa kipindi cha miaka mitano ijayo.

Pia Denmark inatarajia kutumia chombo cha biashara cha fedha cha Shirika la Maendeleo la Denmark kusaidia uhitaji wa uwekezaji wa zaidi ya Krona ya Demmark milioni 500 (DKK) katika miundombinu

endelevu ya kiuchumi, ikianzia katika sekta ya uchukuzi na nishati. Uwekezaji huu unatarajiwa kuboresha ufanisi wa nishati, ulinzi wa mazingira ya bandari na maeneo ya pwani na uboreshaji wa mfumo wa usafirishaji katika maeneo ya vijijini na katika jamii maskini.

Kwa masharti nafuu, kuna uwezekano mzuri wa kuendeleza mfungamano imara wa kibiashara kati ya Denmark na Tanzania. Kilimo na uzalishaji wa chakula, pamoja na teknolojia ya uchumi wa kijani, maji, nishati na ujenzi vinawakilisha baadhi ya maeneo ambayo yanaweza kuwavutia wawekezaji na wasafirishaji wa nje wa Denmark. Ugunduzi wa hifadhi ya nishati pia utatoa fursa za uwekezaji, na huduma kutoka nje zitaendelea kuwa muhimu. Kuzingatia uwezo mdogo wa manunuzi katika sekta binafsi za Tanzania, manunuzi ya umma yatabaki kuwa muhimu katika eneo hili.

Msukumo mkubwa wa sera za kigeni za Tanzania ni kukuza na kuimarisha uhusiano wa kiuchumi wa ndani na nchi za nje. Hii inachukua nafasi chini ya sera za kigeni za uchumi wa kidiplomasia. Wakati uhusiano wa kiuchumi kati ya Tanzania, China na India unaendelea kwa kasi na imara, kuna pia uwezekano mkubwa na utayari wa kuimarisha uhusiano wake wa kiuchumi na wadau wengine, ikiwemo Denmark. Kufikia mwaka 2018, Denmark inatarajiwa kuongeza mara mbili zaidi ya kusafirisha nje na huduma na bidhaa kwa Tanzania. Katika sekta ya huduma, hii itakuwa ya kwanza katika eneo la usafirishaji majini.

Kuimarisha uadilifu wa kikanda unatazamiwa kuimarisha maslahi ya makampuni ya Denmark, njia ya kikanda ya kuifikia Tanzania na Jumuiya ya Afrika Mashariki itaipa mwanya mkubwa wa masoko, ufanyaji biashara wa kikanda na uwekezaji, uwezekano wa kufaidika kutokana na taratibu za ukiritimba wa kodi katika Jumuiya ya Afrika Mashariki na kanuni za forodha. Pamoja na uimarishaji huu, hata hivyo Jumuiya ya Afrika Mashariki hasa Tanzania si soko rahisi kwa Makampuni ya Denmark kuingia. Ni muhimu kuwa na ufahamu wa kisiasa, kijamii na mazingira ya utamaduni. Uvumilivu wa kutosha na mtazamo wenye nguvu wa kukabiliana na vikwazo vya ukiritimba na rushwa vinaweza kuwa kikwazo kikubwa kwa mafanikio. Ubalozi wa Denmark nchini Tanzania umejiandaa kuyasaidia makampuni ya Denmark kuwa na ufahamu katika eneo hili.

Viwango vya ukuaji wa Tanzania pia vinawavutia wawekezaji wa Ulaya, wanaokabiliwa na ukuaji mdogo wa masoko ya ndani katika nchi zao. Aidha, masoko yaliyopo kwa bidhaa za kawaida Tanzania yanaendelea kuwa madogo. Ingawa nchi za Afrika Mashariki zimekuwa na ukuaji wa tabaka la kati, ni muhimu kukumbuka kwamba linaibuka kutoka ngazi ya chini, na kwamba bidhaa zinazozalishwa Ulaya bado ni ghali sana kwa watu wengi katika Afrika Mashariki. Kwa kuzingatia ukuaji wa haraka katika ukanda huu, aidha masoko yanaweza kuchagua baadhi ya bidhaa za kawaida, na kuwa kivutio katika kipindi cha miaka 5 -10, na sasa wawekezaji wa nje wanajiandaa kwa maendeleo haya.

Wizara ya Mambo ya Nje ya Denmark itaendelea kukuza biashara na shughuli za kibiashara kati ya Denmark na Afrika Mashariki, ikiwemo Tanzania. Historia ya muda mrefu ya Denmark kushirikiana na Tanzania ina maana kwamba Ubalozi una nafasi imara kusaidia kwa mapana makampuni ya Denmark katika wigo wa kisekta. Denmark itajitahidi kujenga umoja kati ya ushirikiano wa maendeleo na shughuli za kibiashara kwa kutumia uzoefu wa ushirikiano wa maendeleo katika sekta husika. Ubalozi wa Denmark nchini Tanzania unalenga kujiweka katika nafasi ya kuwa mshauri wa kuigwa kwa makampuni katika kanda kwa kuwezesha kuvutiwa kibiashara na kufaidika kutokana na zana na nyenzo zote za kimataifa. Kwa

### MPANGO WA DENMARK KUCHANGIA MALENGO YA KITAIFA KATIKA MAENEO HAYA:

1. Kuanzisha ajira, hasa kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.
2. Kupunguza ukosefu wa ajira kufikia nusu ifikapo mwaka 2015 ikilinganishwa na kiwango cha mwaka 2008.

jinsi hii, Denmark itatumia mbinu za kina kwa kutumia maendeleo ya ushirikiano, nyenzo za kibiashara na mijadala ya kisiasa kuendeleza zaidi ushirikiano wa kibiashara kati ya Denmark na Tanzania.

## 3.3 KUIMARISHA DEMOKRASIA NA UTAWALA BORA, UTAWALA WA SHERIA NA KUHESHIMU HAKI ZA BINADAMU

Wakati serikali ya Tanzania kwa kiasi kikubwa imejitolea kuhakikisha kutokubagua, kushiriki, uwazi na uwajibikaji katika sekta ya umma, maendeleo katika kutambua kiini cha mabadiliko ya mifumo ya sekta za umma, hazifikii matarajio. Msukumo wa awali wa mabadiliko utahitaji kuanzia kwa wanaowajibika kwa ufasaha wa hali ya juu wakihitaji zaidi uwajibikaji katika mfumo wa kisiasa na uongozi wa kisiasa.

**3.3.1 Eneo Lengwa**

**Kusaidia Upande wa Mahitaji ya Utawala Bora na Haki za Binadamu kwa Wote**

Mkataba wa maendeleo pamoja na serikali ya Tanzania unahusika na upande wa uenezaji wa huduma na utawala kwa watu. Kama nyongeza ya mantiki kwa upande huu wa shirika la maendeleo, pia Denmark itasaidia upande wa mahitaji- asasi za kiraia za Tanzania- kufanya kazi ili kukuza demokrasia, utawala bora, utawala wa sheria na kuheshimu haki za binadamu. Kuna kiungo muhimu kati ya utoaji wa msaada wa bajeti inayoiwezesha serikali kutekeleza majukumu yake, na msaada katika kazi za asasi za kiraia katika kuongeza ufahamu na mahitaji ya kuongeza uwajibikaji katika jamii.

Denmark itasaidia mashirika binafsi ya wananchi, kama vile uanzishaji wa asasi za jamii, katika kuhakikisha kwamba maskini wanakua na sauti katika jamii na kuimarisha taratibu za ufuatiliaji na utetezi katika sekta ya jamii. Haki za wanawake na usawa wa kijinsia ni sehemu zinazoingiliana na ajenda hii, ambazo zina mikakati mikubwa muhimu katika uhusiano kuongezeka kwa watu, moja ya changamoto muhimu kwa Tanzania. Kwa hiyo, eneo hili litakuwa la maana katika juhudi za Denmark kusaidia asasi za kiraia za Kitanzania.

Inatarajiwa kwamba msaada utakwenda hasa kwa taasisi na mashirika muhimu ambayo yanaweza kutetea na kudai utawala bora, kusaidia kuhakikisha mfumo unaowiana ulio muhimu kwa jamii ya kidemokrasia wa kuifanya serikali iwajibike kwa wananchi wake. Mojawapo ya taasisi hizi ni bunge, vyama vya kiraia, (yakiwemo mashirika ya wanawake na watoa msaada wa kisheria), vyombo vya habari na taasisi za sekta binafsi kama vile umoja wa wafanyabiashara na vyama vya wafanyakazi. Denmark watachagua wadau ambao wataweza kusimimia uwajibikaji na uwazi serikalini na mitaani hasa katika kuzingatia matumizi ya rasilimali za umma. Uchaguzi pia utahusisha wadau ambao watalenga kuhakikisha huduma za msingi za kijamii zitawafika wote na hasa wanawake. Wanawake wana mahitaji maalumu katika sehemu ya uzazi wa afya, eneo muhimu sana kwa mpango wa muda mrefu wa maendeleo ya Tanzania. Hatua maalumu zinaweza kubuniwa kuendeleza malengo yaliyo sawa huko Zanzibar, kwa namna nyingine ni jambo muhimu na ambalo lina taasisi zake pekee na pia taasisi zake binafsi.

Malengo makuu na matokeo yanayotarajiwa kwa Denmark kushiriki katika eneo hili:

- Kuimarisha uhitaji wa utawala bora kupitia nguvu na mijadala ya asasi za kiraia.
- Maendeleo ya demokrasia zaidi na ya kina kupitia taasisi imara na uwiano ulio sawa.

### MPANGO WA DENMARK KUCHANGIA MALENGO YA KITAIFA KATIKA MAENEO HAYA:

1. Kukuza amani, mshikamano wa kijamii, mjadala wa kitaifa na utaratibu wa utatuzi wa migogoro (kufikia mwaka 2015);
2. Athari za kupunguza rushwa na fedha bandia (ikifika mwaka 2015);
3. Haki za jamii, siasa, uchumi na utamaduni kwa wote, kwa malengo mahususi kwa wanyonge (kufikia mwaka 2015).

- Kuheshimu sana utawala wa sheria na haki za binadamu.
- Kuboresha uwazi na uwajibikaji kupitia uwezo wa nguvu za taasisi muhimu.

Ili kufanikisha malengo haya Denmark watatumia mijadala ya pamoja na utaratibu wa msimamo wa haki za binadamu kwa kuzingatia mwingiliano wa maendeleo yote.

**3.3.2 Eneo Lengwa**
**Amani na Utulivu wa Kikanda**
Denmark inasaidia upande wa mahitaji ya utawala bora na haki katika jamii ya Tanzania, lakini ikihakikisha maendeleo ya kidemokrasia ya amani, lazima iwe msingi wa kukuza amani na utulivu wa kikanda kama sharti la kuanzisha mazingira endelevu kwa ukuaji wa uchumi, maendeleo ya kijamii na utulivu wa kisiasa. Kwa hiyo Denmark itasaidia na kufanya kazi kwa ushirikiano wa karibu kikanda na masuala ya kimataifa katika maeneo ambayo Tanzania na Denmark itafaidika kutoka kutokana na ushirika.

Kwa kawaida Tanzania imekuwa mshiriki muhimu katika sera za kigeni katika Afrika. Tanzania inaendelea na kawaida hii - kidiplomasia na zaidi ya askari 2,000 wa kulinda amani katika maeneo yenye migogoro. Tanzania iko mstari wa mbele katika mambo ya kimataifa. Demokrasia yake yenye nguvu, msimamo wa kisiasa na ukuaji endelevu wa kiuchumi vimeipa Tanzania jukwaa la utetezi na mamlaka katika kanda na shughuli za kimataifa. Kutokana na hayo imekuwa na uwezo wa kufanyika mshirika imara kwa Denmark. Zaidi ya utetezi wa kimataifa, Tanzania itaweza kukuza ushirika katika mambo muhimu ya kimataifa kama mabadiliko ya hali ya hewa, haki za binadamu, zikiwemo haki za wanawake, ugaidi na uharamia.

Itakuwa hasa katika Umoja wa Mataifa (UN) na vikao vya kimataifa kuwepo uwezekano wa ushirikiano. Tanzania, nchi yenye maendeleo makubwa, huchangia maadili na nchi ndogo iliyoendelea kama Denmark, na kwa kiasi kwamba nchi hizi mbili zinaimarisha ushirikiano wao katika masuala ya kimataifa katika usahihi wa mabaraza haya, itaongeza umuhimu na uhalali wa masuala haya. Kama fursa zinavyojitokeza, Denmark itachochea kutafuta kuimarisha ushirikiano wa karibu na Tanzania katika kuelezea changamoto wanazoshiriki.

Uongezekaji wa jukumu hili muhimu kwa Tanzania katika juhudi za kimataifa za kupambana na uharamia kunatoa fursa maalumu kwa ajili ya ushirikiano. Hivi karibuni Tanzania imeimarisha nguvu za kukabiliana na uharamia, na uwezekano wa mafunzo yanaohitajika kwa ushirikiano wa kikanda katika kukabiliana na uharamia. Hivi karibuni Tanzania na Denmark zimeingia mkataba wa kuondoa uharamia unaodhaniwa kuwepo. Matokeo yake maombi ya Tanzania kwa Denmark yanaweza kukubalika kwa kuhamisha mtu aliyewekwa kizuizini na kikosi cha majini cha Denmark akiwa na tuhuma za uharamia. Mamlaka ya Tanzania yatakuwa na uwezo wa kufanya uchunguzi wa kisheria na kimahakama. Mkataba huu ni ushahidi kwamba Tanzania imechukua wajibu mkubwa pamoja katika mapambano dhidi ya uharamia, na Denmark imejiandaa kuongeza mazungumzo na msaada wa kiufundi mpaka mwisho. Hata hivyo, Tanzania inashiriki vema katika kazi za kimataifa kupambana na uhalifu pamoja na ukatili wa halaiki na kujaribu kukwepa mashitaka na kukuza heshima kwa utawala wa sheria.

**MPANGO WA DENMARK KUCHANGIA MALENGO YA KITAIFA KATIKA MAENEO HAYA:**

1. Kuimarisha ushikariano wa kimataifa na kuweka amani, kutatua migogoro kidiplomasia
2. Kudhibiti uhamiaji, jitihada za ukaguzi wa uingizaji wa silaha haramu na kupambana na vurugu za kuvuka mipaka na uhalifu.

# 4. KUONGEZEKA KWA USHIRIKIANO WA KUBADILISHANA UTAMADUNI

Kila ushirikiano wenye maana kati ya mataifa lazima uhusishe kubadilishana utamaduni kama njia ya kuwaleta raia pamoja na kuimarisha kutambuana pamoja na kufahamiana.Ushirikiano wa Denmark na Tanzania zitaweka msisitizo zaidi juu ya ushirikiano wa utamaduni, na msisitizo maalumu utawekwa katika kufanya sanaa, kwa uwezo wa kufikia sehemu kubwa ya watu katika nchi zote mbili. Msaada wa kuifanya sanaa katika Tanzania unaoweza kuwa na mambo ya kibiashara zaidi. Programu za utamaduni zitaendelezwa na kutekelezwa na Kituo cha Utamaduni na Maendeleo cha Denmark.

# 5. UTAFITI

Kuna utamaduni wa muda mrefu na wenye mafanikio ya utafiti wa ushirikiano kati ya Denmark na Tanzania. Ushirikiano kati ya vyuo vikuu ulianza katika miaka ya 1960 na ulikuwa ni mwanzo wa ushirikiano wa maendeleo. Ushirikiano huu wa maendeleo kwa Denmark na Tanzania umedumu kwa miaka 50, na umeleta matokeo mengi chanya na mazuri, katika mfumo wa kuelimishana wa nchi hizi mbili na uwezeshaji maendeleo katika Tanzania. Denmark itaendelea kusaidia utafiti Tanzania, kwa kupitia utafiti wa maendeleo ya utamaduni na kuwa na ari nyingine ya utafiti kama, utafiti wa ushirikiano wa mwelekeo wa Kusini na ari iliyohusishwa zaidi moja kwa moja na mipango ya sekta.

# 6. MCHAKATO WA UFUATILIAJI

Kwa kila eneo lililodhamiriwa, viashiria maalumu vya ufuatiliaji na matokeo vitachaguliwa. Kwa kiwango kikubwa iwezekanavyo, viashiria hivi vitachaguliwa kutokana na mikakati na taratibu ya serikali ya Tanzania kwa kuhimiza ufuatiliaji katika maeneo yaliyochaguliwa. Denmark itaendeleza ufuatiliaji wa maendeleo na maendeleo dhidi ya viashiria hivi na kukagua kiasi gani msaada umefanikisha matokeo yaliyokusudiwa. Katika kila eneo, Denmark itatambua uwezekano wa hatari na mikakati itahitajika kuendelea kufuatilia na kusimamia hatari hizo. Kiwango cha juu cha uchambuzi wa sera yote ya Denmark na Tanzania na mpango wa nchi utafanyika katika kipindi cha 2014-2018. Lengo litakuwa kutathmini kama malengo mkakati yaliyomo katika kila eneo lililodhamiriwa linaendelea kuwa sawa kulingana na malengo yote kwa jumla, na kama msaada wa Denmark umetolewa kwa njia ya ufanisi zaidi ili kufanikisha matokeo yaliyokusudiwa.

# KIAMBATANISHO CHA 1
# UKWELI KWA TANZANIA

| DATA MUHIMU ZA KIUCHUMI | KIZIO | | CHANZO |
|---|---|---|---|
| Eneo | $km^2$ | 885,800 | WDR |
| Idadi ya Watu (2011) | Milioni | 46.22 | WDR |
| GDP (2011) | Bilioni USD | 23.87 | WDR |
| Ukuaji wa uchumi kwa mwaka (GDP) (2011) | % | 6.45 | WDR |
| GNI kwa kila siku (2011) | USD | 540 | WDR |
| Ukuaji katika GNI kwa kila siku (2011) | % | 3.53 | WDR |
| Urahisi wa ufanyaji biashara (2012) | Daraja | 134 | DB |
| Sekta za Uchumi: Nyongeza ya Thamani (% of GDP) (2011) | | | WDR |
| Kilimo | % | 27.68 | |
| Viwanda | % | 25.07 | |
| Uzalishaji | % | 10.23 | |
| Huduma, n.k. | % | 47.25 | |
| Matumizi ya Serikali (% of GDP) (2010/2011) | % | 27.0 | IMF |
| Kodi ya mapato (bila misaada, % of GDP) (2010/2011) | % | 15.2 | IMF |
| msaada rasmi halisi wa maendeleokwa kila siku (2010) | Iliyopo USD | 65.97 | WDR |
| Msaada rasmi halisi wa maendeleo (% of GNI) (2010) | % | 13.08 | WDR |
| Huduma za mikopo (mgao wa biashara nje – TDS/XGS) (2011) | Mgao | 1.97 | WDF |

| DATA MUHIMU ZA KIJAMII | KIZIO | | CHANZO |
|---|---|---|---|
| Ongezeko la idadi ya watu(wastani wa mwaka) (2000-2010) | % | 2.8 | UGS |
| Matarajio ya kuishi (2011) | Miaka | 58.15 | WDR |
| Vifo vya watoto wachanga (namba ya vifo kwa watoto 1000 mwaka wa kwanzan) (2011) | | 45.4 | WDR |
| Idadi ya watu wenye uwezo wa kupata vyanzo vya maji vilivyoboreshwa (2010) | % | 54.5 | NBS |
| Uwezo wa kupata huduma za afya (asilimia bila uwezo) (mwaka) | % | N/A | HDR |
| Namba ya madaktari (kwa wakazi 100,000 ) (mwaka) | ... | N/A | HDR |
| Watu kati ya miaka 15-49 wanaoishi na VVU (2011) | % | 5.8 | UNAIDS |
| Kiwango cha elimu ya watu wazima (2010) | % | 73.2 | WDR |
| Elimu ya msingi (asilimia ya shule-umri watoto wanaoenda shuleni) (2007)** | % | 83.6 | NBS |
| Wasichana katika elimu ya msingi (asilimia ya wasichana wenye umri wa kwenda shuleni) (2007)** | % | 86.1 | NBS |
| Sekta za kijamii (asilimia ya matumizi ya umma) (mwaka) | % | N/A | WDR |
| Matumizi ya jeshi (asilimia ya GDP) | % | 1.08 | WDR |
| Mgawanyo wa mapato (asilimia ya mapato ya taifa (2007) | | | WDR |
| Tajiri zaidi 10% ya idadi ya watu | % | 29.61 | |
| Maskini sana 10% ya idadi ya watu | % | 2.82 | |
| DATA MUHIMU ZA MAZINGIRA | KIZIO | | CHANZO |
| Kiwango cha eneo la ardhi kilicholindwa kudumisha anuwai ya kibailojia kwa jumla ya eneo lote | % | N/A | CBD/IUCN |
| Kaboni dioksaidi inayotolewa na mtu na matumizi ya ozone – yanayopungua sana CFCs (ODP tons) | Tani za ODP | N/A | UNFCCC |
| DATA ZA HAKI ZA BINADAMU | KIZIO | | CHANZO |
| Uthibitisho wa vyombo muhimu vya haki za binadamu za kimataifa (12 kwa ujumla) | No. | N/A | OHCHR |
| Ridhaa katika vyombo muhimu vya haki za binadamu vya kimataifa | No. | N/A | OHCHR |

Kidokezo: Namba katika jedwadi hili zinaweza kutofautiana kidogo kutokana na namba zilizotumika katika rasimu hii ya sera kutokana na utumiaji wa vyanzo vya kimataifa. Pale inapopatikana, rasimu ya sera imetumia mahesabu mapya ya kitaifa.

# KIAMBATANISHO CHA 2 SHUGHULI ZA MAENDELEO ZA DENMARK KATIKA TANZANIA

**Msaada wa Bajeti Kuu**
Msaada wa moja kwa moja Denmark katika bajeti ya Tanzania unaanzia mwanzoni kabisa mwa ushirikiano wa nchi hizi mbili. Hata hivyo, Msaada wa Bajeti Kuu ya Tanzania katika muundo wake wa sasa ulianzia baada ya Tanzania kufikia msamaha wa kimataifa wa kufutiwa madeni mnamo mwaka 2001, ambapo Denmark ilikuwa mmojawapo wa wadau wa kwanza wa maendeleo kuingia katika mpango wa Bajeti ya Msaada ya Kupunguza Umasikini (PRBS). Lengo kubwa muhimu la msaada huu wa bajeti kuu ni kuchangia katika ukuaji wa uchumi na kupunguza umaskini kwa kusaidia Mikakati ya Kupunguza Umaskini ya Tanzania. Tangu mwaka 2011, Denmark imetoa msaada wa Krona za Denmark (DKK)takribani bilioni 1.1 katika bajeti kuu kwa Tanzania. Pia kiasi cha Krona za Denmark DKK millioni 615 zimeahidiwa kutolewa katika awamu hii ya nne ya mpango wa Denmark wa GBS, ambao unaanza mwaka 2011 mpaka 2015. Katika awamu hii ya sasa, 80% ya mfuko wa fedha wa Denmark unatolewa kwa kiwango kisichobadilika, ambacho ni takribani asilimia ishirini (20%) inategemea kwa kufikia utekelezaji katika maeneo yaliyochaguliwa.

Utoaji wa GBS, pamoja na ongezeko la kodi ya mapato, umeongeza uwezo wa taifa kuhamasisha rasilimali na ongezeko la matumizi ya utumishi wa umma, kwa kuwezesha ukuaji muhimu katika utumishi wa umma, hasa katika afya na elimu. GBS imeunda muundo wa mazungumzo kati ya wadau wa maendeleo na serikali ya Tanzania. Katika suala la upunguzaji umaskini, hata hivyo mchakato umekuwa si wa kuridhisha, kwa kiasi kikubwa kisichobadilika, kiwango kikubwa cha umaskini katika muongo uliopita. Changamoto kubwa za baadaye ni kupunguza gharama za awali za misaada na kuwa na dira ya mazungumzo ya maeneo yenye matatizo, kama vile kupunguza umaskini.

**Demokrasia, Haki za Binadamu na Utawala Bora**
Msaada wa Denmark katika demokrasia, haki za binadamu na utawala bora unaweza kuonekana tangu kuondolewa kwa mfumo wa chama kimoja mwaka 1992. Uchaguzi wa urais wa mwaka 1995 pia ulisaidiwa na Denmark. Kwa miaka mingi Denmark imekuwa ikisaidia maendeleo ya demokrasia Tanzania kwa kuunga mkono taasisi za demokrasia, asasi za umma na maboresho muhimu katika sekta za utumishi wa umma, kama vile mageuzi muhimu katika taasisi za utumishi wa umma, mageuzi katika serikali za mitaa, mageuzi katika usimamizi wa fedha za umma na mageuzi katika sekta ya sheria. Katika awamu iliyopo sasa kuanzia mwaka 2011 mpaka 2015 kiasi cha Krona za Denmark (DKK) milioni 250, zitatolewa kusaidia maeneo matatu. 1) Kuunga mkono ushirikiano wa kidemokrasia na uwajibikaji katika taasisi za utumishi wa umma, na kuviwezesha vyombo vya habari. 2) Kuunga mkono sekta ya vyombo vya sheria kwa kuongeza fursa ya huduma katika vyombo vya sheria na kusaidia mageuzi katika sekta ya sheria. 3) Kuunga mkono programu ya mageuzi katika usimamizi wa fedha za umma ili kufikia mfumo endelevu na imara wa fedha, hasa mfumo endelevu katika usimamizi wa kodi.

**Afya**
Lengo la Denmark kusaidia sekta ya afya ni kufanya maboresho katika sekta ya afya na ustawi kwa Watanzania wote, na kuweka mkazo kuhusu wanawake, watoto na makundi ya Pembezoni. Mpango unaenda sambamba na mkakati wa kitaifa wa upunguzaji umaskini wa Malengo ya Maendeleo ya milenia. Tangu Serikali ya Tanzania ilipoanzisha maboresho ya afya mwaka 1996, msaada wa Denmark umekuwa katika mfumo wa kusaidia mipango kisekta. Awamu ya nne iliyopo ya Msaada wa Mpango sekta ya Afya (HSPS IV) inaanzia mwaka 2009-2014. Programu inasaidia katika maeneo matatu, Sekta ya Afya Tanzania Bara, sekta ya afya Zanzibar na misaada katika sekta mbalimbali za VVU/UKIMWI. Awamu ya nne iliyopo ina jumla ya bajeti ya DKK milioni 910,000,000, ambapo Tanzania Bara inapokea sehemu kubwa ya DKK milioni 528 (80% kwa kupitia mfuko wa pamoja wa Afya). Kwa miaka mingi ya kujihusisha katika sekta ya afya Tanzania Bara na Zanzibar, kumeleta matokeo chanya katika mfumo wa kupunguza vifo vya watoto, kupunguza kiwango cha maambukizi ya magonjwa na mipango bora na ushirikiano katika kusaidia huduma za afya. Changamoto zinaendelea katika kuhakikisha nyenzo ya rasilimali watu na vifaa katika huduma ya afya hasa maeneo ya vijijini, katika utoaji mzuri wa huduma bora na usawa katika upatikanaji.

**Sekta ya Barabara**
Tangu mwishoni mwa mwaka 1980, Denmark imesaidia sekta ya barabara zaidi ya Krona za Denmark (DKK) bilioni 1.9, na kusaidia ujenzi wa baadhi ya barabara muhimu za Tanzania. Upitiaji wa mwaka 2000 ulionyesha nia ya kuwa na mipango ya kijamii, kiuchumi, na kuwa na kipaumbele cha kutoa nafasi kwa ajili ya barabara na watembea kwa miguu. Wakati huo huo, mkazo utakuwa juu ya kuweka vipimo vya usalama barabarani. Barabara na uchukuzi vimepewa kipaumbele cha juu katika mipango ya Serikali katika kupunguza umaskini, na mtandao mzuri wa barabara ni kigezo kinachochukuliwa kwa ukuaji wa uchumi na maendeleo ya kijamii Tanzania. Msaada wa Denmark katika sekta hii utaondolewa polepole ifikapo mwaka 2014.

**Kilimo**
Katika miaka ya 1999 mpaka 2008 Denmark imechangia Krona za Denmark (DKK) takriban milioni 454 za Msaada katika Mpango wa Sekta ya Kilimo. Lengo la jumla ilikuwa kiwango cha ongezeko endelevu la ukuaji wa kipato kwa watu wa vijijini. Ili kufanikisha hili, awamu ya pili ya msaada (ASPS II) ulitolewa kama sera ya mageuzi, uendelezaji wa ukuaji wa sekta binafsi katika sekta ya kilimo (PASS), wakulima kuwa na fursa ya upatikanaji wa mbegu bora na kuongeza maendeleo ya kilimo katika ngazi ya vijijini. Kama muda unavyoendelea kupita ndivyo, vipengele mbalimbali viliendelea kutekelezwa kwa kugawanyika, miradi binafsi, ikikosa mshikamano na mbinu mikakati. Kusudi la kuendeleza uhusiano kati ya vipengele vilivyopotea, hivyo programu haikufanikiwa kulingana na kuwa na athari katika sera ya taifa ya maendeleo, na msaada wa Denmark uliondolewa mwaka 2008. Baadhi ya mambo yenye mafanikio zaidi ni kama msaada wa PASS, baada ya maboresho, sekta ya mipango ya biashara iliongezwa.

**Sekta ya Biashara**
Denmark imekuwa ikisaidia sekta ya biashara na sekta binafsi za maendeleo tangu mwanzoni mwa miaka ya 1980. Madhumini makubwa ya msaada wa Denmark yamekuwa ya kuendeleza sekta binafsi kama injini dhidi ya ukuaji mbovu wa uchumi ambao unasaidia mkakati wa Kupunguza Umaskini Tanzania. Awamu hii ya tatu ya Msaada wa Sekta ya Biashara (BSPS) unalenga kwenye: maboresho katika mazingira ya biashara, kuwezeshwa kuingia katika masoko ya kimataifa na biashara ndogo ndogo; na za kati katika sekta ya biashara pamoja na kilimo. Awamu ya tatu itamalizikia (2008-2013), na uanzishaji wa awamu ya nne utakuwa ni hatua ya mwisho. Jumla ya gharama za msaada kwa awamu tatu za kwanza ni Krona za Denmark (DKK) milioni 925, na awamu ya nne itakuwa na bajeti ya Krona za Denmark (DKK) milioni 600. Awamu tatu za mwanzoni zimeonyesha matokeo muhimu na yametoa mchango mkubwa kwa mfano, uanzishaji wa Elimu ya Ufundi na Mamlaka ya Mafunzo, maboresho katika utendaji wa soko la ajira, kuimarisha uwezo wa Wizara ya Viwanda na Biashara na maboresho ya upatikanaji wa fedha kwa zaidi ya watu milioni moja. Misaada kwa mtazamo mpana wa mageuzi katika mazingira ya kibiashara yamekuwa na mafanikio madogo, na hatua za kawaida za mageuzi zimebaki kuwa pole pole na kuendelea kuwa changamoto kwa wakati ujao.

Shughuli za maendeleo katika sekta ya biashara ya Tanzania inajuimuisha programu ya wadau wa biashara wa Shirika la Maendeleo la Denmark (DANIDA) na misaada kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC). Madhumuni ya misaada kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki ni kuongeza ushirikiano wa uchumi wa kikanda na kuanzisha masoko makubwa, kuongeza ushindani katika soko la kimataifa na kuvutia wawekezaji wa kigeni. Msaada wa sasa wa kiasi cha Krona za Denmark (DKK) milioni 160 zilitolewa katika miaka ya 2012-2014.

**Mazingira**
Denmark imeisaidia Tanzania katika sekta ya mazingira kwa zaidi ya miaka 20. Katika miaka ya 1990 msaada ulianza kutolewa katika miradi ya nyanda za juu kusini, na mwishoni mwa miaka ya 1990, Programu ya Msaada wa Mazingira ulianzishwa, na tangu mwaka wa 2000 ni programu hii ambayo imeipa Denmark mwongozo wa kusaidia. Msaada wa hivi karibuni umelenga katika mambo mawili: 1) Usimamizi wa mazingira ya mijini kwa lengo la kuanzisha mipango ya mazingira na utawala katika ngazi ya Manispaa. 2) Usimamizi wa Maliasili kusaidia misitu na ardhi oevu. Msaada wa programu ulianza mwaka 2007 mpaka 2012 na umekuwa na bajeti ya jumla ya Krona za Denmark milioni 180. Hivi karibuni Denmark imesaidia Tanzania maendeleo ya kwanza ya mikakati ya kitaifa ya mabadiliko ya hali ya hewa. Msaada wa Denmark kwa sekta ya mazingira utaondolewa polepole hadi kufikia mwaka 2015.

**Utamaduni**
Kutoka mwaka 2008 hadi 2012, Denmark imesaidia katika kulinda, kukuza na kuendeleza kitambulisho cha utamaduni pamoja na anuwai Tanzania kwa kiasi cha Krona za Denmark (DKK) milioni 6.2. Katika kufanya kazi na watoto wa shule na wanasanaa wanaojitokeza, msaada unasaidia kuyawezesha makundi yanayoishi katika mazingira magumu kupitia ushiriki wao katika kazi za sanaa na utamaduni. Awamu mpya inatarajiwa.

**Jinsia**
Denmark imesaidia kuwawezesha wanawake wa Tanzania tangu mwaka 2002. Lengo limekuwa katika shughuli za utetezi na kuimarisha haki za wanawake, kwa mfano, elimu na ardhi. Katika awamu iliyoanzia mwaka 2009-2011, moja ya matokeo muhimu yalikuwa ni kukamilika kwa mafunzo ya kitaifa ya uchunguzi wa kijinsia. Awamu ya sasa (2012-2014) kiasi cha Krona za Denmark (DKK) milioni 25, kilitolewa kwa malengo ya kuzuia na kupambana dhidi ya unyanyasaji wa kijinsia na kuwawezesha wanawake kiuchumi, hasa wanawake wa maeneo ya vijijini, kwa njia ya mitandao na kuwaongezea ujuzi wa biashara.

# KIAMBATANISHO CHA 3
# TATHMINI YA MAENDELEO MILLENIA KATIKA TANZANIA BARA KUELEKEA MALENGO YA MAENDELEO YA

| VIASHIRIA | Msingi 1990 | Kiwango cha sasa | Malengo ya MMM(MDG) 2015 | Maendeleo |
|---|---|---|---|---|
| LENGO LA 1<br>KUTOKOMEZA UMASKINI ULIOKITHIRI NA NJAA | | | | |
| 1.1 Idadi ya watu chini ya ($1, PPP) (kulingana na kiwango cha umaskini cha pato la taifa) | 39% | 33.6% (2007) | 19.5% | Yasiyofikiwa |
| 1.1 Idadi ya watu chini ya ($1, PPP) (kulingana na kiwango cha umaskini na kiwango cha umaskini cha pato la taifa) | 21.6% | 16.6% (2007) | 10.8% | Yasiyofikiwa |
| 1.8 Uzito wa chini ya-5 (%) (uzito-wa-miaka -2SD) | 28.8% | 16.8% (2009) | 14.4% | Yasiyofikiwa |
| 1.8 Kudumaa chini ya-5 (%) urefu –wa-chini ya umri wa -2SD) | 46.6% | 38.9% (2009) | 23.3% | Yasiyofikiwa |
| LENGO LA 2<br>KUFANIKISHA ELIMU YA MSINGI KWA WOTE | | | | |
| 2.1 Uwiano halisi wa uandikishaji katika elimu ya msingi (%) | 54.2% | 95.4% (2010) | 100% | Yaliyofikiwa |
| 2.2 Uwiano mkubwa wa uandikishaji wa elimu ya msingi (%) | | 112.7% | 100% | Yaliyofikiwa |
| LENGO LA 3<br>KUHAMASISHA USAWA WA JINSIA NA UWEZESHAJI WA WANAWAKE | | | | |
| 3.1 Uwiano wa wasichana na wavulana katika shule za msingi (%) | 98% | 101% | 100% | Yaliyofikiwa |
| 3.2 Uwiano wa wasichana na wavulana katika shule za sekondari (%) | | 105% | 100% | Yaliyofikiwa |
| 3.3 Uwiano wa wanawake na wanaume katika elimu ya juu (%) | | 68.0% | 100% | Kuelekea kufikiwa |
| 3.4 Uwiano wa wanawake miongoni mwa Wabunge (%) | | 30.3% | 50% | Kuelekea kufikiwa |
| LENGO LA 4<br>KUPUNGUZA VIFO VYA WATOTO | | | | |
| 4.1 Kiwango cha vifo vya watoto chini ya miaka mitano (kwa watoto 1,000 waliohai) | 191 | 81 (2010) | 64 | Yaliyofikiwa |
| 4.2 Kiwango cha vifo vya watot wachanga (kwa watoto 1,000 waliohai) | 115 | 51 (2010) | 38 | Yaliyofikiwa |
| 4.3 Uwiano wa watoto waliochanjwa surua (%) | | 85% | 90% | Kuelekea kufikiwa |

| VIASHIRIA | Msingi 1990 | Kiwango cha sasa | Malengo ya MMM(MDG) 2015 | Maendeleo |
|---|---|---|---|---|
| LENGO LA 5<br>KUBORESHA AFYA YA UZAZI | | | | |
| 5.1 Uwiano wa vifo vya wajawazito (kwa watoto waliohai 100,000) | 529 | 454 (2010) | 133 | Yasiyofikiwa |
| 5.2 Uwiano wa waliozalishwa na wataalamu wa afyal (%) | 43.9% | 50.5% (2010 DHS) | 90% | Yasiyofikiwa |
| LENGO LA 6<br>KUPAMBANA NA VVU/UKIMWI, MALARIA NA MARADHI MENGINE | | | | |
| 6.1 Maambukizi ya VVU, miaka, 15-24 (%) | 6% | 2.5% (2008) | ‹ 6% | Yaliyofikiwa |
| Maambukizi ya VVU miaka 15-49(%) | | 5.7% (2008) | ‹ 5.5% | |
| LENGO LA 7<br>KUHAKIKISHA MAZINGIRA ENDELEVU | | | | |
| 7.8 Uwiano wa watu wanaotumia vianzo vya maji ya kunywa vilivyoboreshwa (% ya wakazi wa vijijini) | 51% | 57.1% (2009) | 74% | Yasiyofikiwa |
| 7.8 Uwiano wa watu wanaotumia vianzo vya maji ya kunywa yaliyoboreshwa (% ya wakazi wa mijini) | 68% | 83% (2009) | 84% | Yaliyofikiwa |
| 7.9 Uwiano wa watu wenye fursa za kuboresha usafi wa mazingira (Mijini/Vijijini) | | 13.3% (2010 DHS) | | Yasiofikiwa |
| LENGO LA 8<br>KUENDELEZA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA KWA AJILI YA MAENDELEO | | | | Kueleka kufikiwa |

Chanzo:Ripoti ya nchi ya malengo ya maendeleo ya millennia 2010, http//www.porvertymonitoring.go.tz/

Denmark – Tanzania:
Rasimu ya Sera ya Nchi 2014 – 2018
Juni 2014

Mtayarishaji:
Wizara ya Mambo ya Nje ya Denmark
Asiatisk Plads 2
1448 Copenhagen K
Denmark

Simu +45 33 92 00 00
Nukushi +45 32 54 05 33
Baruapepe um@um.dk
Tovuti www.um.dk

Mbunifu: BGRAPHIC
Picha, ukurasa wa mbele: Mikkel Østergaard
Ramani: Umoja wa Mataifa

Chapishi linapatikana kutoka:
www.danida-publikationer.dk

Uchapishi uliyomo unaruhusiwa kunakiliwa.

ISBN: 978-87-7087-794-7 (toleo kwa tovuti)

MINISTRY OF FOREIGN AFFAIRS OF DENMARK

DANIDA | INTERNATIONAL DEVELOPMENT COOPERATION

WWW.DANIDA.DK